**Mghwira** afariki dunia, Rais Samia atoa rambirambi

UKURASA 2



**Mama** adai kuibiwa kichanga baada ya kujifungua mapacha

UKURASA 7




UCHUMI

**PASS TRUST**

**Wabia serikalini 'PPP' waliloweka kambi Dodoma 2021 kueneza Kilimo Biashara**

- Nusu wanufaika kinamama; ajira milioni 2.5
- Miradi 46,300 na wajasiriamali milioni 1.7



UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Julai 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580650

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


LIKE & FOLLOW US


# Kinachoendelea dhidi ya Mbowe

**Akataa** kutoa maelezo polisi, RPC aomba radhi, CHADEMA yatoa tamko... *Endelea ukurasa 2*

## Tony Blair aiahidi Tanzania misaada

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Waziri Mkuu mstaafu wa Uingereza, Tony Blair, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



Mwonekano wa mitaa inayolizunguka Soko Kuu la Kariakoo, jijini Dar es Salaam ikiwa wazi baada ya vibanda vya wafanyabiashara wadogo vilivyojengwa kiholela kuondolewa. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Shahidi aeleza Sabaya alivyovamia, kupora fedha

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA ZAAMSHA SHANGWE** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Tony Blair aiahidi Tanzania misaada

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu mstaafu wa Uingereza, Tony Blair, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, ilisema Blair ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi ya Mabadiliko Ulimwenguni (Tony Blair Institute for Global Change) amemhakikishia Rais Samia kuwa taasisi yake inaunga mkono jitihada mbalimbali anazochukua katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania.

Alisema taasisi yake inafanya kazi katika nchi 16 Afrika ikijikita kutekeleza vipaumbele vya serikali zao na kusema katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu taasisi yake imejikita zaidi katika masuala ya kukabiliana na janga la UVIKO 19.

Blair alisema katika kukabiliana na janga la UVIKO 19, taasisi yake inashughulika zaidi na masuala ya upimaji na usambazaji wa chanjo na taasisi yake inaweza kusaidia Tanzania kuwafikia wazalishaji wa chanjo hizo.

Pia wanajengea uwezo nchi washirika kufuatilia miradi ya kilimo, nishati na matumizi ya teknolojia.

Kwa upande wake Rais Samia amemshukuru Blair kwa kumjulisha masuala yanayofanywa na taasisi yake katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika nchi washirika.

Rais Samia alisema kwa sasa serikali inaendelea na uboreshaji wa mazingira bora ya uwekezaji kwa sekta binafsi, ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) wa Tanzania.

Kuhusu UVIKO 19, Rais Samia alimweleza Blair kuwa tayari serikali ina mpango wa kitaifa kuhusu namna ya kushughulikia masuala yote ya UVIKO 19 ikiwamo uratibu wa chanjo.

Rais Samia alisema katika kujijengea uwezo kwa sasa serikali ina mpango wa kujenga viwanda vya kuzalisha chanjo za aina mbalimbali na hivyo kuomba taasisi ya Tony Blair kuunga mkono jitihada hizo.

Aidha, Rais Samia ameikaribisha Taasisi ya Tony Blair kuja nchini kufanya kazi na taasisi za Tanzania kusaidia utekelezaji wa vipaumbele vya serikali.



Mafundi wakiendelea wa upanuzi wa barabara ya Kilwa, eneo la Mtoni Mtongani, mkoani Dar es Salaam jana. Kutokana na ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya barabara ya mabasi ya mwendokasi kutoka Mbagala hadi Gerezani, eneo hilo limekuwa likisababisha foleni kubwa ya magari na usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kinachoendelea dhidi ya Mbowe

**Na Waandishi Wetu**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, amewaomba radhi waandishi wa habari kwa kutowapa ushirikiano katika tukio la kukamatwa kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake jijini Mwanza.

Vilevile, amesema jeshi hilo limempeleka Mbowe Dar es Salaam linakodai anakabiliwa na tuhuma zingine na akimalizana nao, atarudishwa jijini Mwanza.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda Ng'anzi alisema kuwa kama binadamu, alifanya makosa na kuwaomba radhi waandishi wa habari waliohudhuria mkutano huo.

Alidai kuwa juzi kulikuwa na kazi nyingi jijini Mwanza na yeye kama binadamu, inawezekana alishindwa kutoa ushirikiano wa kutosha kwa waandishi wa habari waliotaka kujua kinachoendelea baada ya Mbowe na wenzake kukamatwa usiku wa manane wakiwa hotelini.

Juzi Kamanda Ng'anzi hakutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari na ilipofika jioni alipokea simu ya mwandishi wa Nipashe na kujibu kwa kifupi na kisha kukata simu.

Akizungumzia kukamatwa kwa Mbowe, Kamanda Ng'anzi alisema kuwa baada ya kumkamata jijini Mwanza, juzi alfajiri alisafirishwa kwenda Dar es Salaam ili kuhojiwa kwa tuhuma zingine zinazomkabili.

Kamanda Ng'anzi alitaja baadhi ya watuhumiwa wanaoshikiliwa kuwa ni pamoja na aliyekuwa Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mwenyekiti wa sasa wa Baraza la Vijana (BAVICHA), John Pambalu na wengine 13.

Hata hivyo, taarifa ya maandishi iliyotolewa na Kamanda Ng'anzi kwa waandishi wa habari, hakikuwa na jina la Mbowe kwenye orodha ya watuhumiwa 15 waliokamatwa na jeshi hilo jijini Mwanza.

Alisema upelelezi ukikamilika, watuhumiwa hao watapelekwa mahakamani kujibu tuhuma kama zitakuwapo.

Jijini Dodoma, CHADEMA Mkoa wa Dodoma jana walitishia kufanya maandamano yasiyo na kikomo endapo Jeshi la Polisi halitamwachia Mbowe pamoja na viongozi wengine wanaowashikilia.

Katibu wa chama hicho mkoani humo, Mathias Nyakapala, alitoa kauli hiyo alipozungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano wake uliofanyika ofisi za kanda za chama hicho.

Nyakapala aliwataka jeshi hilo kumwachia Mbowe bila masharti yoyote na kama hawatafanya hivyo watafanya maandamano kuanzia leo yasiyo na kikomo hadi watakapowaachia.

"CHADEMA Mkoa wa Dodoma tunalitaka Jeshi la Polisi kumwachia Mbowe bila masharti yoyote, wasipofanya hivyo mpaka leo (jana) saa 10 jioni, tutaanza maadamano yasiyo na kikomo mpaka watakapowaachia," alisema.

Jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alidai Mbowe alifikishwa Dar es Saalam juzi majira ya saa tatu usiku na alipelekwa hadi nyumbani kwake Mikocheni kwa ajili ya upekuzi uliochukua takribani saa mbili na nusu.

Mrema alidai kuwa baada ya upekuzi, askari polisi walichukua kompyuta mpakato mbili, vishikwambi vya watoto wake na moderm kwa ajili ya uchunguzi wao.

"Majira ya saa saba mchana leo (jana), polisi walimfikisha Mbowe Kituo Kikuu cha Polisi kwa ajili ya mahojiano. Polisi walitaka maelezo kutoka kwa Mbowe kuhusiana na kosa walililoiita 'kula njama za kutenda kosa la ugaidi'," alidai.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mrema, Mbowe alitumia haki yake ya kisheria, akikataa kutoa maelezo yoyote kisha akarejeshwa Kituo cha Polisi Oysterbay.

Alidai kuwa viongozi wengine wanaendelea kushikiliwa jijini Mwanza na baadhi wamefanyiwa upekuzi majumbani kwao na hoteli walizokuwa wamefikia jijini humo.

●**Imeandaliwa na Richard Makore (MWANZA), Ibrahim Joseph (DODOMA) na Romana Mallya (DAR)**

# Rais Samia amlilia Anna Mghwira

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kufuatia kifo cha aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira.

Mghwira alifariki dunia jana katika Hospitali ya Rufani ya Mount Meru mkoani Arusha alipokuwa akipatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, Rais Samia alisema amepokea taarifa za kifo cha Mghwira kwa majonzi na masikitiko makubwa hasa akikumbuka mchango wake mkubwa alioutoa katika ujenzi wa taifa.

Aliwaomba wanafamilia wote wawe na moyo wa uvumilivu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi na amemwombea marehemu Anna Mghwira apumzike mahali pema peponi.

Mghwira aliwahi kuwa Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo taifa na mwaka 2015 aligombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya chama hicho na kushika nafasi ya tatu nyuma ya mgombea wa CCM, Hayati Dk. John Magufuli na aliyekuwa mgombea wa CHADEMA, Edward Lowassa.

Baada ya uchaguzi huo Rais Magufuli alimteua Mghwira kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, wadhifa aliodumu nao hadi hivi karibuni Rais Samia alipoteua wakuu wapya wa mikoa, huku nafasi yake ikijazwa na Stephen Kigaigai.

HABARI KITAIFA

# Shahidi aeleza Sabaya, wenzake walivyovamia duka, kuchukua pesa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa pili wa upande wa Jamhuri, Numan Jasini (17), katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (pichani), jana alipanda kizimbani kukamilisha ushahidi wake.

Julai 20, mwaka huu, shahidi huyo alishindwa kufika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Arusha ambako kesi hiyo inaendelea kunguruma, kutokana na sababu za kiimani kwa kuwa ilikuwa sikukuu ya Eid el Haji.

Katika kesi hiyo inayosikilizwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo, Sabaya (34) na wenzake wawili, Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha. Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, alimhoji shahidi huyo kama ifuatavyo;-

**Swali:** Baada ya mabaunsa wa Sabaya kumweka chini ya ulinzi na kumsachi Bakari Msangi nini kiliendelea?

**Jibu:** Wakati wakimpiga Bakari Msangi, Sabaya alikuwa anamwambia kwamba amekwenda kuwasaidia magaidi wenzake na Bakari alikuwa anapiga kelele kuomba mshamaha lakini waliendelea kumpiga. Aliwaambia walinzi wake wampige kipigo kizito sana na Bakari aliishiwa nguvu na kulala chini.

**Swali:** Nini kilichosababisha alale chini?

**Jibu:** Baada ya kipigo aliishiwa nguvu na Sabaya aliagiza wamsimamishe na kumkalisha.

**Swali:** Nini kiliendelea baada ya kumkalisha?

**Jibu:** Sabaya alitoa silaha aina ya bastola na kumnyooshea huku akimwambia atammaliza kwa kuwa ana kiherehere sana na Bakari aliomba wasimuue kwa sababu mke wake na mtoto ni wagonjwa sana. Baada ya hapo, Sabaya aliwaagiza walinzi wake kumfungua pingu Bakari kwa kuwa alikuwa amefungwa pingu kama walivyoagizwa.

**Swali:** Hebu ieleze mahakama ni wakati gani Bakari alifungwa pingu?

**Swali:** Wakati akiwa chini ya ulinzi alifungwa pingu na baunsa.

**Swali:** Ni nani alitoa agizo la kufungwa pingu?

**Jibu:** Agizo la kufungwa pingu lilitolewa na kiongozi wao ambaye ni Sabaya.

**Swali:** Baada ya kufunguliwa pingu nini kiliendelea?

**Jibu:** Bakari aliendelea kuomba msamaha na miongoni wao alisogea karibu na mimi kuniambia nimpigie simu Abuu Mansuri.

**Swali:** Kwa nini alikwambia umpigie simu Abuu Mansuri?

**Jibu:** Alisema kuna biashara alifanya naye kwa pamoja na yule dada aliyekwenda kununua bidhaa Februari 8 na 9, mwaka huo.

**Swali:** Na wakati ukipiga simu huyo dada alikuwa wapi?



**Jibu:** Alikuwa chini ya ulinzi.

**Swali:** Na ulipompigia simu Abuu Mansuri alikwambiaje?

**Jibu:** Alisema hawezi kuja dukani kwa kuwa hajisikii vizuri na muda ulikuwa umekwenda.

**Swali:** Baada ya majibu hayo nini kiliendelea au kilitokea?

**Jibu:** Sabaya alichukua simu yangu na kumwambia Abuu Mansuri nakupa dakika tano uwe umefika hapa. Baada ya alikata simu na aliniambia kwamba nimpigie Mohamed Saad, na akifika atatuachia huru kwa kuwa hatuhitaji sisi.

**Swali:** Baada ya kukwambia umpigie ulimpigia?

**Jibu:** Nilimpigia hakupatikana na nilimjibu hivyo na Sabaya aliniambia nitafute namna yoyote na nilimwomba atuachie. Alinijibu kwamba mhusika akifika hapo dukani atatuachia huru

**Swali:** Baada ya hapo nini kiliendelea?

**Jibu:** Aliagiza mabaunsa wake waniweke chini ya ulinzi na kunilazimisha niendelee kupiga simu.

**Swali:** Baada ya kukuweka chini ya ulinzi nini kiliendelea?

**Jibu:** Aliniambia nimpigie tena simu Mohamed Saad, nilipiga simu lakini haikupatikana, hivyo aliniambia nimpige tena Abuu Mansouri.

**Swali:** Baada ya kukwambia umpigie simu nini kiliendelea?

**Jibu:** Mjomba wangu Hajirini Saada alisema yeye atampiga simu Abuu Mansuri.

**Swali:** Wakati huo Hajirini Saada yeye alikuwa wapi?

**Jibu:** Tulikuwa naye chini ya ulinzi hapo dukani.

**Swali:** Je, baada ya Hajini kusema atapiga simu nini kiliendelea?

**Jibu:** Alipiga simu na baada ya muda Abuu Mansuri alifika dukani.

**Swali:** Alipofika nini kiliendelea?

**Jibu:** Alifunguliwa mlango na kuingia na baada ya hapo walimweka chini ya ulinzi na kumsachi.

**Swali:** Umesema kwamba Msangi alishikiwa silala. Baada ya hapo nini kilitokea?

**Jibu:** Mmoja wa walinzi walichukua silaha hiyo na kututishia na kutushachi.

**Swali:** Kwa hiyo unataka kuieleza mahakama kwamba silaha ilihama kutoka kwa Sabaya na kwenda kwa mlinzi wake?

**Jibu:** Ndio. Baada ya hapo waliendelea kumhoji Abuu Mansuri.

**Swali:** Sabaya alimwambiaje Abuu Mansuri?

**Jibu:** Sabaya alimwambia Abu Mansuri huyu dada unamfahamu na Februari 8 ulikwenda naye wapi? Alimwambia kwamba alimsindikiza benki kubadilisha fedha

**Swali:** Je, Sabaya alimjuaje Abuu Mansuri?

**Swali:** Mmoja wa walinzi wake walikuwa na faili lenye picha ambayo inamwonyesha huyo dada akiwa amefuatana na Abuu Mansuri.

**Swali:** Baada ya kumhoji kwa muda Abuu Mansuri nini kiliendelea?

**Jibu:** Sabaya ambaye ndio kiongozi aliwaagiza walinzi wake kumpiga ili kumtoa 'lock' Abuu Mansuri.

**Swali:** Katika ushahidi wako huko awali ulisema kuna mtu anaitwa General huyu ndio alisema Abuu Mansuri apigwe na huyu General ni nani?

**Jibu:** Ndio, General (Sabaya) ndiye alitoa agizo hilo na baada ya hapo aliagiza Abuu kupigwa kipigo kizito na walipomaliza aliagiza afungwe pingu moja na Bakari Msangi na walinzi hawakufahamu namna ya kuwafunga na kiongozi wao akawa anawaelekeza kufunga.

**Swali:** Baada ya kuwaelekeza namna ya kufunga pingu?

**Jibu:** Sabaya alitoka na baadhi ya walinzi wake walifunga mlango na wengine walibaki ndani dukani wakiendelea kupekua duka.

**Swali:** Wakati huo Bakari Msangi na Abuu Mansuri walikuwa wapi?

**Jibu:** Tulikuwa nao ndani wakiwa wamefungwa pingu na waliwekwa mbele yetu.

**Swali:** Baada ya kiongozi wao kutaka na kurudishia duka nini kiliendelea?

**Jibu:** Aliporejea alianza kuwaachia watu waliowekwa chini ya ulinzi akiwamo Ali, Mzee Salimu, Abuu Mansuri, Bakari Msangi.

**Swali:** Hebu isaidie mahakama katika ushahidi wako. Umesema Sabaya aliagiza Bakari na Mansuri nini kiliendelea baada ya kufungwa pingu moja?

**Jibu:** Baada ya muda General Sabaya, aliporejea aliagiza wafunguliwe pingu waliokuwa wamefungwa mikononi.

**Swali:** Baada ya watu kuruhusiwa kuondoka nini kiliendelea dukani kwenu?

**Jibu:** Sabaya aliendelea kunihoji mimi na mjomba wangu Hajirini Saad huku wakiendelea kupekuwa na kuchukua nyaraka na mashine za kielektroniki EFD na kuchukua baadhi ya simu ambazo walizichukua kwa watu waliowapekua.

Pia waliendelea kupekua kaunta lakini sikuona walichochukua kwa kuwa nilipokuwa nimekaa ingekuwa vigumu kuwaona niliona walichukua simu na nyaraka zilizokua juu ya meza

**Swali:** Hapo kaunta walipokuwa wanasachi mnawekaga nini?

**Jibu:** Kuna masanduku mawili moja la kuweka fedha za mauzo na lingine nyaraka.

**Swali:** Je, moja ya masaduku hayo siku hiyo yalikuwa na kiasi gani cha fedha?

**Jibu:** Sanduku la kuhifadhia fedha siku hiyo lilikuwa na Sh. 2,769,000

**Swali:** Je, ulijuaje kuna kiasi hicho cha fedha?

**Jibu:** Tayari nilikuwa nimeshafanya hesabu na kufahamu kiasi cha pesa kilichokuwapo kwenye sanduku.

**Swali:** Je, uliiambia mahakama baada ya hapo mmliambiwa mfunge duka ilikuwaje?

**Jibu:** Tulifunga duka tukisimamiwa na walinzi wa kiongozi huyo na tulipotoka nje tulimuona sehemu akiwa anaangalia dagaa. Mjomba wangu Hajirini akamwomba Sabaya amnunulie ndizi mbivu kwa kuwa alikuwa amefunga na alitununulia ndizi mbili moja yangu na nyingine ya mjomba wangu. Baada ya hapo walinzi walitusimamia tukapanda kwenye gari.

**Swali:** Je, mlipandishwa kwenye gari wewe na nani?

**Jibu:** Tulipanda kwenye gari mimi na Hajirini tukiwa na Sabaya na walinzi wake watatu, mmoja akiwa kwenye gari upande wa dereva na wengine walikaa nyuma.

**Swali:** Baada ya kuingia kwenye gari nini kiliendelea?

**Jibu:** Msafara wa magari matatu ulitoka tukaanza kuzungushwa mitaa ya Soko Kuu na Bondeni kisha wakatupeleka hadi karibu na jengo la nyumba yetu.

**Swali:** Baada ya kufika nyumbani kwenu nini kiliendelea?

**Jibu:** Alishuka mmoja wa walinzi wakaanza kuulizia geti la kuingilia kwetu.

**Swali:** Baada ya kuulizia nini kilitokea?

**Jibu:** Mmoja wa walinzi walinipatia simu yangu wakaniambia nipige simu nyumbani wafungue mlango.

**Swali:** Baada ya kuambiwa hivyo ulifanya nini?

**Jibu:** Nilimpigia mama yangu kumwambia asifungue mlango na wakati huo Sabaya alikuwa nje ya geti letu.

**Swali:** Wakati unaletewa simu kuambiwa upige kule kwenye gari ulikuwa na nani?

**Jibu:** Nilikuwa mimi mjomba wangu na walinzi watatu wa Sabaya.

**Swali:** Upo katikati ya walinzi watatu ukaambiwa upige simu ulipata wapi ujasiri wa kuzungumza hayo?

**Jibu:** Nilizungumza kwa lugha ya kiarabu hivyo hawakuelewa nimemwambiaje. Baada ya kuzungumza hayo niliwaeleza kwamba simu ya mama yangu haipatikani kwa mmoja wa walinzi. Tuliondoka na msafara wa magari matatu kuelekea Kituo Kikuu cha Polisi cha Arusha.

**Swali:** Baada ya kuingia kituo cha polisi nini kiliendelea?

**Jibu:** Kiongozi huyo alishuka kwenye gari na kuzungumza na askari na baadaye tuliandika maelezo. Tulipomaliza tuliambiwa tumeachiwa kwa dhamana na siku ya Februari 10. Tulitakiwa kuripoti kituoni majira ya saa 10:00 jioni tukiwa na Mohamed Saad.

**Swali:** Baada ya kupatiwa dhamana nini kiliendelea?

**Jibu:** Tulipewa simu zetu mimi na Hajirini Saad na askari aliyechukua maelezo yetu alitupa lifti ya kutubeba kwa kutumia gari lake mpaka nyumbani kwetu.

**Swali:** Kwa kusaidia mahakama wakati mnaambiwa mfunge duka ilikuwa majira gani?

**Jibu:** Nakumbuka giza lilikuwa limeshaanza kuingia na sikumbuki ilikuwa saa ngapi.

**Swali:** Hawa watu ambao walikuja dukani kwenu ukiona utawatambua?

**Jibu:** Ndio nitawatambua watu hao kwa kwa kuziangalia sura zao na miili yao.

**Swali:** Pale waliposimama askari magereza pembeni yao, kuna watu watatu wamekaa. Je, umeshawahi kuwaona popote au unawafahamu?

**Jibu:** Watu hawa watatu ndio walikuja dukani kuvamia Februari 9.

**Swali:** Kuna watu uliwatambua waliofika dukani?

**Jibu:** Wa kwanza ni Ole Sabaya alikuwa kiongozi wao akitoa maagizo yote. Wa pili ni Sylvester alinikabidhi simu yangu kuwaambia watu wa nyumbani wafungue mlango na watatu ni Daniel tulipanda naye gari moja.

**Swali:** Je, mtu wa kwanza na wapili pale dukani uliweza kuwatambua?

**Jibu:** Kwa pale dukani sikuweza kumtambua mtu wa kwanza wa pili na watatu kutokana na vurugu zilizotokea hapo dukani. Lakini nilipotoka nao nje ya duka niliwatambua vizuri wote.

**Swali:** Na mliporejeshwa nyumbani nini kilitokea?

**Jibu:** Ferbuari 10 majira ya saa 10:00 nilipokea simu kutoka kwa Bakari Msangi. Anieleza kwamba natakiwa kwenda kituo cha polisi kuandika maelezo kutokana na tukio lililotokea Februari 9 na baadaye nilimwambia baba yangu akanisindikiza kwenda kituoni. Nilimkuta askari anayeitwa Onuku aliandika maelezo.

**Swali:** Je, baada ya kuandika hapo nini kilitokea? **Jibu:** Kutokana na kutokea kwa jambo hilo, tulikwenda kuomba kibali polisi cha kufungua duka. Baada ya hapo Februari 12, Ali Saad, mimi kwa pamoja na askari polisi (Onuku), tulifungua duka.

**Swali:** Hebu ieleze Mahakama baada ya kifungua duka mlikuta katika hali gani?

**Jibu:** Tulikuta vitu vimevurugika yakiwamo makapeti na pembeni ya kaunta kulikuwa na damu.

**Swali:** Kwa upande wa kaunta na vitu mlivyoviacha ilikuwaje?

**Jibu:** Tulipoangali baadhi ya nyaraka na fedha za mauzo Sh. 2,769,000 hatukuzikuta kwenye sanduku la kuwekea hela.

**Swali:** Baada ya kwenda polisi nini kilifuata?

**Jibu:** Baada ya polisi kufanya upelelezi wao Februari 12, kwa kuwa muda ulikuwa umekwenda, Februari 13 tuliruhusiwa kufungua duka kuendelea na biashara.

**Swali:** Baada ya kufungua nini kilichofuata nini kilitokea?

**Jibu:** Nilijaribu kumpigia mjomba wangu Mohamed Saad sikumpata kwenye simu. Lakini Februari 17 alinipigia mwenyewe na nilimweleza kiasi hicho cha fedha kilichoibiwa.

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | UK Holding Company Limited, S.L.P 3215, Dar es salaam. | Eneo la Keko Mwanga, Mtaa wa Depoit – Temesa, Wilaya ya Temeke, Dar es salaam | John Msigwa (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi (Lubricant) |
| 2. | Sun Shine Mining Limited, S.L.P. 31299, Dar es Salaam. | Eneo la kijiji cha Konkilanki, Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida. | Heilongjiang Liaoning (Mchina) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 3. | Kioo Limited, S.L.P. 9273, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 180, Eneo la Chang'ombe, Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam | Kumar Krishnan (Mhindi) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 4. | Oliver Rishaely Kaaya Dabalo, S.L.P. 15374, Arusha. | Eneo la Kijiji cha Dabalo, Kata ya Dabalo, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma. | Oliver Rishaely Kaaya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta Kijijini |
| 5. | Oryx Morocco Service station, S.L.P 9540, Dar es salaam. | Kiwanja Na.27, Eneo la Ursino South, Manispaa ya Kinondoni, Dar es salaam. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Unique Petroleum Tanzana Ltd- Mabama, S.L.P. 119, Tabora. | Eneo la Kijiji cha Mabama, Barabara ya Urambo, Kata ya Mabama, Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora. | Shaffin Sumar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 7. | Samo Christopher Roche-Bukene, S.L.P. 872, Musoma. | Eneo la Kijiji cha Bukene, Kata ya Bukene, Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora. | Samo Christopher Roche (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 8. | Kinyalla General Traders, S.L.P 2185, Arusha. | Kijiji cha Muriet, Kata ya Sokoni 1, Halmashauri ya Jiji la Arusha, Mkoa wa Arusha. | Aloyce Ephrahim Mosha (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Ketumbeine Filling Station, S.L.P 84, Longido. | Kijiji cha Armanie, Kata ya Ketumbeine, Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha | Eliud Loitu Mollel (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Ntanyinya Fuel Filling Station – Saza, S.L.P 101, Chunya. | Kijiji cha Saza, Wilaya ya Songwe, Mkoa wa Songwe. | Fidel A. Ntanyinya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | Delldeta Refueling, S.L.P 35691, Dar es Salaam. | Kijiji cha Mpepai, Wilaya ya Mbinga, Mkoa wa Ruvuma. | Nurubicco Charles Mponda (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 12. | Gudal (T) Co. Ltd-Msamvu, S.L.P. 216, Nzega. | Kiwanja Na. 328, Kitalu "B", Eneo la Msamvu Mwembesongo, Wilaya ya Morogoro, Mkoa wa Morogoro. | Hassan Mussa Abdillah (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 13. | Darpco Energy Co. Ltd, S.L.P. 3892, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2024, Kitalu "K", Eneo la Mbezi, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es salaam. | Thabit George Mkasi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 14. | Energy Oil Bamaga, S.L.P. 106125, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 572, Kitalu "43", Eneo la Kijitonyama, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es salaam. | Sood mohamed Sood (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 15. | Amer Mohamed Mbarak, S.L.P. 13656, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1028, Kitalu "V", Eneo la Sokota, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es salaam. | Amer Mohamed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 16. | Hass Petroleum (T) Ltd Geita Service Station, S.L.P. 78341, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 41, Kitalu 'M', eneo la Mbugani - Geita Mjini, Wilaya ya Geita, Mkoa wa Geita | Abdulkadir Ahmed Hussein (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 17. | Fly Petrol Station, S.L.P. 480, Musoma. | Kiwanja Na. 80, Kitalu "B", eneo la Makutano Trading Center, Wilaya ya Butiama, Mkoa wa Mara. | Mwita Mnanka Ohura (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 18. | Alindas Transport & Oil Products Ltd – Rwambaizi S.L.P. 159, Karagwe | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", eneo la Rwambaizi, Wilaya ya Karagwe, Mkoa wa Kagera. | Amos Daudi Kaihula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 19. | Damian F. Bulunda - Bulunda Oil, S.L.P. 44, Buchosa. | Kijiji cha Bukokwa, Wilaya ya Buchosa, Mkoa wa Mwanza. | Damian Francisco Bulunda (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 20. | Joseph Augustino Mdaka, S.L.P 273, Mbinga. | Kiwanja Na.30, Kitalu "A", Eneo la Tanki la Maji (Masumuni), Mbinga Mjini, Mkoa wa Ruvuma. | Joseph Augustino Mdaka (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |
| 21. | NA, S.L.P. 1484, Iringa. | Eneo la Kitanzini, Barabara ya Jamatini, Iringa Mjini, Mkoa wa Iringa. | Fahmi Omary Awadh (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |
| 22. | Albert Hosea, Iringa Mjini, Iringa. | Eneo la Iringa Mjini, Kata ya Ilala, Iringa Mjini, Mkoa wa Iringa. | Albert Hosea (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |
| 23. | Kisamo Filling Station, S.L.P. 159, Karatu. | Eneo la Singida Mjini, Barabara ya Majengo, Kata ya Majengo, Singida Mjini, Mkoa wa Singida. | Anael Akilimali Kisamo (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya kupikia (LPG) |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

216370302

# TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA NISHATI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

*(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibitiwa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Suraya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 21(4) ya Kanuni za Mafuta (Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Reja Reja na Matumizi Binafsi),Gazeti la Serikali Toleo Na. 817 la 2020)*

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na majina ya kituo kama ifuatavyo: -

1. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Nyegezi Filling Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2017-115.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 138 na 139, Kitalu 'D', Eneo la Nyegezi, Wilaya ya Nyamagana, Mkoa wa Mwanza

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Nyegezi Filling Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

2. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Bukoba Parves Shabirdin Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2017-086.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 142, Barabara ya Bukoba, Wilaya ya Bukoba, Mkoa wa Kagera

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Bukoba Filling Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

3. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Gairo Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-196.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 1 na 2, Kitalu 'P', Wilaya ya Gairo Mjini, Mkoa wa Morogoro

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Gairo Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

4. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Kurasini Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-212.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 2044 na 2045, Kitalu '3', Eneo la Kurasini, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Kurasini Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

5. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Mabatini Filling Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-245.
Mahali Kituo Kilipo: Kiwanja Na. 15, Kitalu 'C', Eneo la Mabatini, Wilaya ya Nyamagana, Mkoa wa Mwanza

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Mabatini Filling Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

6. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Kahama Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-348.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 4, Kitalu 'U', Eneo la Nyasubi, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Kahama Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

7. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Rahaleo Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2020-421.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 200, Kitalu 'H', Barabara ya Tanu, Mkoa wa Mtwara

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Rahaleo Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

8. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Kibada Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2020-416.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 9, Kitalu '14', Eneo la Kibada, Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Kibada Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

9. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Makangarawe Filling Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2021-133.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 167/1, 169/1 na 170, Kitalu 'A', Eneo l a Makangarawe, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Makangarawe Filling Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

10. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Makangarawe Filling Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2020-217.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 699 na 170, Kitalu 'FF', Eneo la Buzuruga - Nyakato, Mkoa wa Mwanza

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Buzuruga Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

11. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Mikocheni Service Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2020-393.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 672, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Mikocheni Service Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

12. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Ngaramtoni Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2021-153.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 1512, Kijiji cha Olorien, Kata ya Ngaramtoni, Wilaya ya Arumeru, Mkoa wa Arusha

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Ngaramtoni Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

13. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Ngarenaro Service Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2017-049.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 47 na 53, Kitalu 'C' Eneo la Ngarenaro, Wilaya ya Arusha, Mkoa wa Arusha

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Ngarenaro Service Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

14. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Ikwiriri Service Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-378.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 477, Eneo la Ikwiriri, Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Ikwiriri Service Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

15. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Sokota Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-108.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 44 na 48, Eneo la Sokota, Mkabala na Barabara ya Mandela, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Temeke Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

16. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Temeke Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2018-109.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 176, Kitalu 'G', Eneo la Temeke Mwisho, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Temeke Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

17. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Chamazi Filling Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-213.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 2083, Kitalu 'D', Eneo la Chamazi, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Chamazi Filling Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

18. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– KDC Kiboriloni Petrol Station
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2017-099.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 1, Kitalu 'A', Wilaya ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– KDC Kiboriloni Petrol Station
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

19. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Tegeta Petrol Station Wazo
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2019-067.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 1082, Kitalu 'H', Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Tegeta Petrol Station Wazo
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

20. **Jina la awali la kituo:** Camel Oil (T) Ltd– Vikindu
**Nambari Ya Leseni:** PRL-2018-488.
**Mahali Kituo Kilipo:** Kiwanja Na. 9, Kitalu 'A', Eneo la Vikindu, Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani

**Jina Linalopendekezwa:** Africa Energy Limited– Vikindu
**Mmiliki Wa Awali:** Camel Oil (T) Ltd
**Mmiliki Mpya:** Africa Energy Limited

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

216370302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utaratibu wa chanjo uwe wazi na shirikishi

**JANA** Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, amesema chanjo zimefika nchini na anayehitaji kuchanjwa yupo huru kuchanjwa wakati wowote, katika vituo maalum vilivyopangwa kwa huduma hiyo.

Aidha, amesema serikali ilichukua uamuzi wa busara wa kuagiza na kuziletea chanjo nchini baada kugundua kuna Watanzania ambao ni wafanyabiashara na wasafiri wa shughuli tofauti nje ya nchi, ambazo sharti upatiwe au kuwa na cheti cha chanjo kuingia nchini mwao.

Pia, serikali ilisema kuna chanjo mbili ambazo zimepitishwa kwa Watanzania kutumia. Hii ni taarifa nzuri kwa umma kwa kuwa sasa wale wanaotaka kuchanja watapata huduma hiyo kwa wakati muafaka.

Ni muhimu sasa serikali iweke wazi hospitali maalum za kutoa chanjo hiyo kwa kuwa wanaotaka kuchanja ni wengi wanasubiri kujua ni wapi pa kwenda, ili kupata huduma hiyo.

Lakini taarifa ni nyingi kuwa ili uchanjwe ni lazima upimwe corona, kama huna ndiyo uchanjwe, kuliko kuchanjwa ukiwa na maradhi hayo mwilini athari zake ni kubwa na husababisha hata watu kupoteza maisha.

Pia, umuhimu wa chanjo kwa kuwa zipo taarifa kuwa ikiwa umechanjwa na unachangamana na wasiochanjwa kuna uwezekano wa kupata maambukizi, huku wengine wakidaiwa kupoteza maisha baada ya kupata chanjo, na wengine wakibaki na athari mbalimbali jambo linaloogopesha watu kufanya uamuzi.

Zipo taarifa kuwa baadhi ya watu huenda wakapoteza maisha, na kuna waliopoteza maisha baada ya kuchanjwa, hizi zote ni taarifa zinazopaswa kuwekwa vizuri kwa umma ili kuwe na uelewa wa kutosha.

Lakini ni muhimu chanjo zikatajwa ili kuondoa minong'ono kuhusu chanjo zinazotumika nchi mbalimbali duniani au zilizoanza kutumiwa kwenye ofisi za kimataifa nchini.

Suala la chanjo limekuwa na maneno mengi huku kukiwa na taarifa nyingi duniani baadhi ya nchi zikisema hazitakubali waliopata chanjo za nchi fulani kuingia nchini mwao, hali inayowalazimu waliochanjwa chanjo ilisiyokubaliwa na nchi nyingine basi wachanjwe kwa kadri ya matakwa.

Tunajua serikali ilituhakikishia kuwa itafanya utafiti wa chanjo kabla ya kukubali ipi inayofaa kutumika nchini, na kuwataka wananchi kuwa watulivu huku mipango ya kujenga kiwanda cha kutengeneza chanjo ikiendelea.

Taarifa zote hizi ni muhimu zikawafikia wananchi na kwa kuwa kuna mpangilio kwenye mamlaka za serikali za mitaa, ni rahisi kufikisha ujumbe kwa umma ili waweze kufanya uamuzi sahihi kwa wakati sahihi kwa manufaa yao.

Ni muhimu elimu hii ikaanzia ngazi ya mtaa, kijiji, kata, tarafa na wilaya kupitia mikutano muhimu ambayo huleta pamoja wananchi, lakini kuwa na mabango yenye ujumbe wa kuelimisha umma lengo ni kuzishinda habari zinazovuma ambazo nyingine siyo za kweli.

Elimu sahihi itawezesha wananchi kupata chanjo kwa wingi kwa kuwa hakuna ubishi kuwa hali ilikofika ni lazima watu kupata chanjo.

Lakini kwa kuwa ni mara ya kwanza inatolewa nchini na inajulikana ni bure basi uwapo utaratibu mzuri kwenye hizo hospitali ili kusije kukazua majanga au kuongeza maambukizi ya ugonjwa huo wakati ingewezekana kuzuia.

Pia, ni muhimu elimu kwa umma ikaendelea kutolewa kwa wingi namna ya kujikinga kwa kuwa bado wananchi wengi hawafuati taratibu za kujikinga na corona, kuanzia kwenye vyombo vya usafiri wa umma, kwenye mikusanyiko na kwingine kokote.

Pia, ni muhimu kuelimisha umma umuhimu wa kufanya mazoezi asubuhi na jioni kwa kuwa ni namna sahihi ya kukabiliana na maradhi hayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Asante Rais kusikia kilio kodi simu, tuvute subira

Na Sabato Kasika

**TOZO** za miamala ya simu iliyoanza kutumika hivi karibuni, iliibua malalamiko kutoka kwa wananchi na kusababisha Rais Samia Suluhu kuguswa nayo ameagiza mawaziri husika kutafuta suluhisho.

Baadhi ya watumiaji simu walilalamikia kuwa makato ni makubwa wakati wa kutuma na kupokea fedha na kuona huduma hiyo kama mzigo mkubwa kwao na kutaka yafanyike mabadiliko.

Miongoni mwa yaliyosemwa na wananchi ni kwamba, huduma ya simu kwa sasa imekuwa ni moja ya huduma muhimu kwa Watanzania, hivyo haipaswi kuongezewa kodi na tozo hizo.

Badala yake, wakaishauri serikali kubuni njia za mapato kwa taifa, ili kuboresha huduma za kijamii kuliko kuumiza wananchi kwa ntozo za simu ambazo baadhi ya watu hawana uwezo wa kuzilipa.

Pamoja na nia nzuri ya serikali ya kuweka tozo hiyo kwa ajili ya kuboresha huduma za kijamii, lakini ushirikishwaji wa Watanzania katika mchakato wa upatikanaji wa sheria hiyo ulikuwa mdogo.

Kutokana na sintofahamu hiyo ya miamala, baadhi ya wananchi wakashauri kwamba serikali ingeweka kiwango cha fedha cha kuanza kukatwa tozo, angalau kianzie miamala ya Sh. 50,000.

Ushauri huo ulilenga kutowatoza Watanzania wa hali ya chini kwenye mzunguko rasmi wa kifedha, pia wakaiomba serikali kupunguza kiwango cha kodi kilichopo kwa kuwa makato yaliyowekwa ni makubwa sana.

Malalamiko hayo yalisababisha Rais aingilie kati na kuagiza mawaziri husika kutafuta suluhisho, ambalo Watanzania wanaendelea kulisubiri ili waendelee kupata unafuu waliokuwa wakiupata kwenye miamala ya simu.

Kwa kuwa Rais ameshaingilia kati, basi ni vyema wananchi kuwa na subira, ili hatimaye malalamiko yao yaweze kupatiwa ufumbuzi ili kuondoa mkanganyiko ambao ulijitokeza siku chache zilizopita.

Wakati kilio hicho kikiwa kinafanyiwa kazi, ipo haja pia ya kutoa elimu ya mlipa kodi ili kusaidia wananchi kutambua umuhimu wake na kuona fahari kulipa kodi, kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Hiyo inatokana na kwamba, ni wajibu wa Watanzania kuhakikisha serikali inakusanya kodi kwao, ili kuwahudumia, kwani ulipaji kodi unawezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Maendeleo ndiyo hitaji kubwa la wananchi, lakini hayawezi kuja bila kulipa kodi, hivyo wananchi wakipata elimu ya kutosha ya mlipa kodi, watalipa bila kusukumwa na hata tozo za miamala halitaleta shida.

Ikumbukwe kuwa ulipaji kodi unasaidia kukuza uchumi wa mtu mmoja na taifa kwa ujumla, pia huduma zote za kijamii zinatolewa kupitia kodi ambazo serikali hukusanya kutoka kwa wananchi.

Lakini, unapotokea utata kama huo ulio kwenye tozo za miamala ya simu, ni wazi kwamba kuna jambo linaloweza kuwa halijakaa vizuri aidha wananchi kutokuwa na elimu ya kutosha ya mlipa kodi, au vinginevyo.

Ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali, shule, miundombinu ya barabara, umeme na mingine mingi, hutegemea kodi, hivyo kila Mtanzania awe na elimu ya mlipa kodi.

Kodi pia inatumika katika mishahara ya watumishi na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya msingi na sekondari bila ada, huduma hizo na nyingine nyingi, ni vyema wananchi wakaelimishwa kujua umuhimu wake.

Vilevile ni vyema kodi ikawa rafiki kwa mlipaji, ili asikwepe wala kulalamika, ingawa inawezekana wakawapo watu wanaolalamika kwa sababu zao nyingine kwa lengo la kutaka kukwepa.

Suala la kuendelea kuwaelimisha Watanzania kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ni la msingi, ili kila mmoja wao aone fahari kuilipa kwa ajili ya maendeleo yake na ya taifa lake kwa ujumla.

Pamoja na hayo, kuwa na subira kwenye tozo la miamala ya simu ni muhimu kwa kuwa kilio kimeshasikika na kinaendelea kufanyiwa kazi, kwa kuzingatia kwamba, subira huwa inavuta heri.

## HABARI KITAIFA

# Adai kuibiwa kichanga alipojifungua mapacha

**Na Mwandishi Wetu, SIMIYU**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, Zawadi Abdallah, mkazi wa Kidinda mjini Bariadi, amedai kuibiwa mtoto na wataalamu wa afya katika hospitali ya halmashauri hiyo (Somanda) alipojifungua watoto wawili.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Mei 23, mwaka huu baada ya Zawadi kwenda hospitalini huko kujifungua, akiambatana na mama yake mzazi, Joyce Lujiga.

Zawadi na mama yake walidai juzi kuwa pia walishangaa kuona wanatakiwa kugharamikia vifaa tiba na dawa ambavyo vilihitajika kwenye upasuaji.

Kwa mujibu wa Zawadi, siku hiyo baada ya kufika hospitalini majira ya mchana, alipimwa na madaktari (majina tunayahifadhi) ambao walimwambia alikuwa na mapacha na alitakiwa kufanyiwa upasuaji. "Baada ya majibu hayo ya vipimo, walimweleza mama yangu (Joyce) kuwa anatakiwa kusaini fomu za kwenda kufanyiwa upasuaji, naye mama akawasiliana na baba yangu na mume wangu wakaruhusu ndipo nikapelekwa chumba cha upasuaji," alisema Zawadi.

Joyce (mama wa Zawadi) alidai kuwa baada ya upasuaji kwenda vyema huku mwanawe (Zawadi) akiwa hajitambui, alishangaa kuona analetewa mtoto mmoja wa kiume badala ya mapacha kama ambavyo waliambiwa awali.

"Kwa kuwa mtoto wangu Zawadi alikuwa hajitambui, nikawauliza mtoto mwingine yuko wapi?

"Daktari huyo huyo aliyetupima mwanzo, akasema 'mtoto ni mmoja, huyo tu, hakuna mwingine, bali alikuwa mkubwa kilo nne."

"Nikabaki ninashangaa na Zawadi baada ya fahamu kurejea, akashangaa anapewa mtoto mmoja," alisema Joyce.

Zawadi aliendeleza madai yao akisema: "Baada ya wiki mbili, nilirudi hospitalini kwa ajili ya kusafishwa kidonda, ndipo nilipokutana na mkunga mmoja jina lake silijui, aliponiona nikiwa nimekaa kwenye benchi ninasubiria huduma huku nikiwa nimebeba mtoto wangu, aliniuliza 'mbona umebeba mtoto mmoja, mwingine yuko wapi?

"Mimi nilimkatalia nikamwambia labda unanifananisha, akasema 'wewe si unaitwa Zawadi?', nikaitikia 'ndiyo', akasema yeye alikuwapo wakati wa upasuaji nilijifungua watoto wawili, nikabaki nashangaa kisha akaondoka."

Alisema kuwa aliporejea nyumbani, alimweleza mama yake kilichotokea na ndipo familia ikaamua kurejea hospitalini kufuatilia ukweli.

"Nilifika kwa viongozi wa hospitali nilichokutana nacho ni majibu ya kejeli tu, wahudumu wote ambao walihusika kwenye upasuaji waliitwa lakini walianza kunishambulia kwa maneno ya kejeli," alidai.

Zawadi pia alionyesha stakabadhi yenye orodha ya vifaa alivyodai kununua kwa ajili ya upasuaji huo vikiwa na thamani ya Sh. 130,000.

Alipotafutwa kuzungumzia suala hilo, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Said Mlowosha, alikiri ofisi yake kupata malalamiko hayo na mama huyo alifika hospitalini kwa ajili ya kujifungua.

Dk. Mlowosha alisema kuwa uchunguzi wa awali taarifa zake kwenye mafaili kuanzia alipopimwa hadi chumba cha upasuaji, zilizonyesha hakuna sehemu ambayo iliandikwa alikuwa na mapacha.

"Taarifa zote kwenye mafaili yake zinaonyesha alikuwa na mtoto mmoja ambaye alikuwa mkubwa uzito wa kilogramu 3.3, lakini tunaendelea na uchunguzi zaidi kubaini ukweli juu ya majibu na hicho kilichotokea," alisema.

Dk. Mlowosha alisema uchunguzi wa kina unaendelea kubaini muuguzi aliyemwambia Zawadi kwamba alijifungua watoto wawili ili kujua kama ni kweli au la.

Kiongozi huyo pia alisema mteja wao huyo kutakiwa kununua baadhi ya vifaa vya upasuaji ni kosa kwa kuwa sera inaelekeza huduma kwa mama wajawazito ni bure, hivyo nalo wanalifanyia uchunguzi.

# Atuhumiwa kuua mke kisa fedha za mahindi

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

JESHI la Polisi Singida linamshikilia Juma Shabani (45) mkazi wa Kijiji cha Ndulungu,wilayani Iramba kwa tuhuma kuua mkewe, Moshi Rashidi (40).

Mtuhumiwa anadaiwa kufanya mauaji hayo kwa kumpiga Moshi kwa kutumia kitu chenye ncha kali, kutokana na ugomvi wa kifamilia kuhusiana na mauzo ya mahindi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, ACP Stela Richard Mutabihirwa, alisema tukio hilo lilitokea Jumapili usiku katika Kijiji cha Ndulungu,wilayani Iramba.

Alisema siku ya tukio hilo mwanamke huyo alipigwa na mumewe kwa kitu chenye ncha kali katika sehemu mbali mbali za mwili.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutabihirwa, uchunguzi wa awali umebaini chanzo kikubwa cha mauaji hayo ni ugomvi wa kifamilia pamoja na ulevi.

Alisema ugomvi ulizuka baada ya Moshi kudai fedha za mahindi yaliyouzwa kwa ajili ya kulipa ada ya mtoto shuleni.

Aidha kamanda huyo alisema baada ya Moshi kudai fedha hizo ndipo mtuhumiwa alipoanza kumshambulia kwa kumpiga kwa fimbo na kitu chenye ncha kali, hivyo kumsababishia kifo.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutabihirwa, baada ya mtuhumiwa kutenda kosa hilo, alikamatwa na anatarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## UNAUDITED RESULTS
### FOR THE SIX MONTHS ENDED 30 JUNE 2021

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

Despite strong competition in the cement manufacturing industry and uncertainties brought about by COVID-19, Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) delivered a strong operating result when compared to the year 2020. Both the sales volume and revenue increased compared to year 2020. Revenue increased by 16% compared to the same period last year.

The operating performance and the availabilty of the plant and machinery was good, thus ensuring clinker production level higher than year 2020, all within an environment where the Health and Safety of our employees and contractors is paramount. The continued focus on delivering excellent customer service, the selling of high quality products, and the belief in maintaining strong customer relationships enabled TPCPLC to again demonstrate its strength as the leading player in the industry.

| INCOME STATEMENT | JAN - JUN 2021 TZS'000 | JAN - JUN 2020 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 210,825,663 | 181,454,388 |
| Cost of sales | (126,277,122) | (113,688,511) |
| **Gross profit** | **84,548,541** | **67,765,877** |
| Other operating income | 821,403 | 2,278,447 |
| Selling and administrative expenses | (1,552,643) | (1,585,357) |
| Administrative expenses | (9,314,386) | (9,315,110) |
| Depreciation and amortisation | (8,681,096) | (8,626,083) |
| Other operating expenses | (1,091,706) | (1,467,018) |
| **Operating profit** | **64,730,113** | **49,050,756** |
| Financial items | 1,298,145 | 1,585,255 |
| **Profit before tax** | **66,028,258** | **50,636,011** |
| Taxes on income | (19,937,458) | (15,692,080) |
| **Profit for the year** | **46,090,800** | **34,943,931** |

| BALANCE SHEET | 2021 TZS'000 | 2020 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Intangible fixed assets | 797,216 | 823,264 |
| Tangible fixed assets | 130,771,416 | 131,529,045 |
| Other non-current assets | 4,286,500 | 10,358,097 |
| **Non.current assets** | **135,855,132** | **142,710,406** |
| Inventories | 69,747,539 | 58,987,795 |
| Trade and other receivables | 60,811,816 | 56,934,604 |
| Cash and cash equivalents | 73,260,020 | 60,817,350 |
| **Current assets** | **203,819.375** | **176,739,749** |
| **TOTAL ASSETS** | **339,674,507** | **319,450,155** |
| **EQUITY & LIABILITIES** | | |
| **Equity** | **230,868,930** | **214,565,616** |
| Lease liabilities | 3,196,726 | 6,610,379 |
| Long term provisions | 6,621,779 | 8,070,602 |
| Provision for deferred taxes | 12,940,597 | 16,188,193 |
| **Non-current liabilities** | **22,759,102** | **30,869,174** |
| Lease liabilities | - | - |
| Current income tax payable | 3,447,885 | 1,568,115 |
| Trade and other payables | 79,801,715 | 69,100,427 |
| Dividend payable | 2,796,875 | 3,346,823 |
| **Current liabilities** | **86,046,475** | **74,015,365** |
| **TOTAL EQUITY & LIABILITIES** | **339,674,507** | **319,450,155** |

**Prospects**

The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPCPLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work to maintain its leadership.

**Appreciation**

The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
Chairman of the Board
15.07.2021

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania**
**www.twigacement.co.tz**
**Email: info@twigacement.co.tz**

216369201

HABARI KITAIFA

## Serikali yatoa tamko samaki waliokufa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeruhusu shughuli za uvuvi kuendelea katika Soko la Kimataifa la Samaki Feri wakati uchunguzi ukiendelea kuhusu samaki waliokutwa wamekufa katika ufukwe uliopo karibu na Hospitali ya Aga Khan na Ocean Road jijini Dar es Salaam.

Jana, Nipashe iliandika habari kuhusiana na samaki hao waliokutwa juzi ufukweni wakiwa wamekufa.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, iliwatoa hofu wananchi na kuwataka waendelee na biashara ya samaki katika soko hilo.

Wizara hiyo iliahidi kutoa taarifa ya uchunguzi wa vifo vya samaki hao mara baada ya kukamilika kwake ili kubainisha kuwa walishateketezwa.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inapenda kuwashukuru wananchi wote waliokuwapo kwenye ufukwe wa Hospitali ya Aga Khan na Ocean Road pamoja na Soko la Magogoni Feri wakati wa tukio hili kwa ushirikiano mkubwa walioonyesha uliofanikisha kuzuia kuingizwa kwa samaki hawa sokoni na hatimaye kuteketezwa na Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam," ilibainisha.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa sampuli za samaki hao zilichukuliwa kwa ajili ya maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Maabara ya Taifa ya Uvuvi (Dar es Salaam) na Jeshi la Polisi Kitengo cha Sayansi ya Uchunguzi kwa ajili ya kupeleka Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Pia taarifa hiyo ilisema baada ya kuimarisha ulinzi eneo la Soko la Magogoni na eneo la tukio, wananchi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, maofisa wa wizara, TAFIRI, maofisa uvuvi wa Halmashauri ya Jiji wakiwa na mameneja wa Soko la Feri, walikusanya kiasi cha kilo 164 na kukifikisha Kituo Kikuu cha Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA), Deogratius Rutatwa (kushoto), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu virusi vya ugonjwa wa Corona (UVIKO-19) kwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU). Katikati ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, Leticia Kapela na Naibu Mtendaji Mkuu wa baraza hilo, Scholastica Williams. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya Leseni ya Kuuza Gesi Asilia iliyoshindiliwa kwa ajili ya kuendeshea magari kutoka kwa Kampuni ya Anric Gas Technology Tanzania Company Limited. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kuhusiana na maombi hayo ya leseni. Taarifa za mwombaji pamoja na maelezo ya maombi ni kama zinavyoelezwa hapa chini:

| | MAELEZO |
|---|---|
| Jina na anuani ya Mwombaji | Anric Gas Technology Tanzania Company Ltd, S.L.P 77819, Dar Es Salaam |
| Eneo la Mtambo | Kiwanja namba 98, Bara bara ya Nelson Mandela/ Kilimo, mtaa wa Usalama, kata ya Sandawal, Manisipaa ya Temeke, Mkoa wa Dar Es Salaam. |
| Taarifa za Wana hisa | 1. Wenjie Guo, 65%<br>2. Qiao Cheng, 25%<br>3. Chao Zheng 10% |
| Maelezo ya Mtambo na Matumizi | Kuuza gesi asilia iliyoshindiliwa kwaajili ya magari yanayo tumia gesi asilia *(Dispensing)* Gesi hiyo itauzwa kwenye kituo kama yanavyo uzwa mafuta ya magari. |
| Aina na Muda wa Leseni | Leseni ya kuendesha kituo cha kuuzia gesi asilia iliyoshindiliwa kwaajili ya magari yanayo tumia gesi asilia *(CNG FSL)* ya muda wa miaka mitano (5) |

216370802

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi haya awasilishe kwa maandishi kabla ya saa 10 jioni ndani ya siku kumi na nne (14) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Maombi ya leseni yanaweza kuonyeshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-4, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz


# Wabaini upotoshaji corona kwa WAVIU

**Na John Badi**

BARAZA la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA), limeitaka jamii kuondokana na taarifa potofu zinazoenezwa juu ya ugonjwa wa virusi vya Corona (UVIKO-19) kwa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU).

Vilevile, baraza hilo limeiomba serikali kutoa elimu ya kutosha juu ya chanjo ya corona kwa makundi mbalimbali hasa kwa WAVIU juu ya upatikanaji, faida, madhara na hata ubora wake ili kujenga msingi mzuri na kumsaidia anayehitaji, kufanya uamuzi sahihi ya kupata chanjo hiyo.

Akitoa tamko la baraza hilojana, Mwenyekiti wa NACOPHA, Leticia Kapela, amesema WAVIU ni sawa na watu wengine, akibainisha kuwa wapo WAVIU waliougua ugonjwa wa corona, lakini kwa kuzingatia tiba sahihi kutoka kwa wataalamu wa afya na kufuata maelekezo, wamepona.

"Eti kwa kuwa watu wanaoishi na VVU (Virusi vya UKIMWI), wanakuwa na upungufu wa CD4 mwilini, hivyo wapo hatarini zaidi wanapopata maambukizi ya corona, jambo ambalo si kweli.

"WAVIU ni kama alivyo mtu yeyote anaweza kukabiliana na ugonjwa huu endapo atafuata kanuni na taratibu za afya kutoka kwa wataalamu," alisema.

Kapela aliwaomba viongozi na taasisi za dini na vyombo vya habari kuhakikisha wanaendeleza jukumu la kutoa elimu sahihi kwa jamii iliyozunguka na umma kwa jumla juu ya UVIKO-19 na pia kuwaondolea wasiwasi kwa taarifa zinazotolewa za kupotosha au kutia hofu Watanzania.

Aliwaelekeza wafanyakazi wote wa baraza, viongozi na waratibu wa kongani za baraza, vikundi wezeshi na familia zao kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo ya wataalamu na tamko la Rais Samia Suluhu Hassan kuwa corona ipo.

"Hivyo, wazingatie maagizo na kuchukua tahadhari zote si mahali pa kazi tu bali hata kwenye makazi yao na jamii kwa ujumla na pia kuwalinda wale wanaowahudumia," alisema.

Aliongeza kuwa baraza limewashauri na kuwaelekeza WAVIU kuhakikisha wanaendelea kupata huduma stahiki za VVU kipindi chote bila kuathiriwa na uwapo wa UVIKO-19 na wanaomba WAVIU kutoa taarifa mara moja pale watakapoona mabadiliko yoyote katika utoaji na upatikanaji wa huduma za afya katika maeneo yao.

Baraza hilo pia limempongeza Rais Samia kwa kuunda kamati maalum ya UVIKO-19 Aprili mwaka huu, ambayo inaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya udhibiti na mikakati mbalimbali ya kinga kulingana na hali ya maambukizi ya UVIKO-19 inavyoendelea duniani kote.

"Ninapenda kutoa rai na kusisitiza kwa WAVIU, familia zetu na Watanzania kwa ujumla ni muhimu kujikinga na ugonjwa huu wa UVIKO-19 maana kinga ni bora kuliko tiba," alihimiza.

## HABARI KITAIFA

# RC Sendiga apiga marufuku makongamano, mikusanyiko

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amepiga marufuku mikusanyiko yakiwamo makongamano kwa maelezo ni mkakati wa kupambana na kasi ya maambukizi ya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari, alisema uamuzi huo unatokana na Iringa kuwa ni miongoni mwa mikoa yenye idadi kubwa ya wagonjwa wa Covid-19.

Sendiga alisema hali si nzuri, hivyo tahadhari inapaswa kuchukuliwa na kila mmoja, kwamba mkoa umeamua kuchukua tahadhari ya kuzuia mikusanyiko.

"Niwaombe wanahabari muendelee kutoa elimu kwa wananchi juu ya janga hili la corona hali si nzuri ndani ya mkoa wetu, idadi ya wagonjwa ni kubwa sana sina mamlaka ya kutoa taarifa ya wagonjwa ila itoshe kusema tahadhari inapaswa kuchukuliwa," alisema Sendiga.

Alisema alishatangaza kuwa kila mwananchi wa Iringa kuvaa barakoa popote anapokuwa hasa kwenye mikusanyiko kama sokoni, kwenye vyombo vya usafiri na maeneo mengine, hivyo ni lazima wananchi kuzingatia agizo hilo. Sendiga alisema ameshakutana na viongozi wa taasisi za dini na makundi mbalimbali kuwaomba kuendelea kuelimisha wananchi juu ya janga la corona na ataendelea kufanya hivyo.

"Hatuwezi kukataza watu kwenda sokoni ama kwenye nyumba za ibada na kwenye shughuli zingine za kiuchumi zinazokusanya watu wengi ... tunachosisitiza ni kwamba kila anayeenda kwenye kusanyiko azingatie kanuni ya kujilinda na kuwalinda wengine," alisema.

Akijibu maswali ya wanahabari kuhusu abiria kwenye vyombo vya usafiri, vikao vya ndani vya vyama vya siasa na mikusanyiko ya nyumba za ibada, Sendiga alisema wenye vyombo vya usafiri lazima kuchukua tahadhari na kwenye nyumba za ibada pia wameelekezwa jinsi ya kuchukua tahadhari, na kwamba vikao vya ndani ya kisiasa anaamini tahadhari zitachukuliwa.

Kuhusu mikusanyiko ya kwenye taasisi za elimu, alisema nako wanapaswa kuendelea kuchukua tahadhari ya corona, huku akisema serikali haitaacha kuchukua hatua kwa yeyote atakayekaidi agizo hilo la mikusanyiko ndani ya mkoa huo.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, akifungua mkutano wa 38 wa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakumbushwa kujihadhari corona

**Paul Mabeja na Renatha Msungu,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amewaomba waumini wa dini mbalimbali nchini kuendelea kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya pamoja na kuchukua tahadhari zote dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona kwenye maeneo ya ibada.

Aliwasihi wasimamizi wa nyumba zote za ibada kuhakikisha kuwa wanaendelea kuwaelekeza waumini wao kujilinda na maambukizi hayo kwa kuweka ndoo za maji tiririka na sabuni.

Shekhe Rajabu, alisema hayo juzi wakati alipokuwa akitoa mawaidha kwa waumini wa dini ya Kiislamu walioshiriki ibada ya Eid al Hajj iliyofanyika katika Msikiti wa Gadaff, jijini Dodoma.

Alisema ugonjwa huo upo nchini na kwamba waumini wa dini hiyo hawana budi kuendelea kuchukua tahadhari zote za kujilinda.

"Ndugu zangu Waislamu ugonjwa huu upo na unaendelea kuua watu hivyo hatuna budi kuendelea kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya," alisema.

Vilevile, aliwataka viongozi wa nyumba za ibada kuendelea kutoa elimu ya kujilinda na virusi vya corona waumini wao.

Aliwataka Watanzania kuendelea kuilinda amani iliyopo nchini pamoja na kuwaombea viongozi wa nchi akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake.

"Nitoe wito kwa waumini wa Kiislamu nchini kuisherehekea sikukuu hii kwa amani na utulivu na kuendeleza mema ambayo tumeyafanya katika siku 10, tulizofunga," alisema Shekhe Rajabu.

Katika hatua nyingine, Shekhe wa Msikiti wa Nunge, Abdul Musa Kondo, alisema wataalamu wa afya waliopewa jukumu la kuagiza chanjo ya ugonjwa huo wahakikishe wanaleta chanzo ambazo hazitasababisha madhara kwa jamii.

Aliwataka wataalamu hao kutumia taaluma zao katika kuwahudumia wagonjwa ikiwamo kuwaelimisha namna ya kujikinga ili wasipate madhara kwa mara nyingine.

Shekhe Kondo akizungumza kwenye sala ya Eid El Haji iliyofanyika Uwanja wa Jamhuri, alisema wataalamu watakaohusika kuagiza chanjo hizo wanapaswa kuwa makini kupata za uhakika kuwa zitawasaidia Watanzania badala ya kuleta bandia zitakazoangamiza maisha ya watu.

"Tunaomba wataalamu msimwangushe rais tafadhali agizeni chanjo ambazo zinauhakika wa kukinga badala ya kuleta madhara," alisema.


## NOTISI / TANGAZO

**NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD, MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, ,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MWANAHAMISI ATHUMAN LUMAJA | MBAGALA | ELVIS ERICK LUYEGO | NYUMBA | VIKINDU HONDA | 11/08/2021 NA KUENDELEA |
| 2 | STEPHANO MARTIN MWARABU | MBAGALA | STEPHANO MARTIN MWARABU | NYUMBA | TOANGOMA | 7/08/2021 NA KUENDELEA |
| 3 | RAJABU SHABANI RAJABU | UBUNGO | RAJABU SHABAN RAJABU | NYUMBA | MBWENI-MPIJI | 10/08/2021 NA KUENDELEA |
| 4 | GODFREY MICHAEL CHUWA | KARIAKOO | GODFREY MICHAEL CHUWA | NYUMBA | KIMARA KING'ONGO DSM | 11/08/2021 NA KUENDELEA |
| 5 | SEGUMBA JAPHARI MHANDO | BUGURUNI | SEGUMBA JAPHARI MHANDO | NYUMBA | VIWEGE 'A' MAJOHE DSM | 12/08/2021 NA KUENDELEA |
| 6 | CHACHA JOHNSON MATIKO | BUGURUNI | CHACHA JOHNSON MATIKO | KIWANJA | CHANIKA KWA WAMBII CENTER | 7/08/2021 NA KUENDELEA |
| 7 | MARIAM PATRICK SHAYO | UBUNGO | DORICE YOHANA MWAKAPESA | KIWANJA | MBEZI MSAKUZI | 10/08/2021 NA KUENDELEA |
| 8 | LUCIANA JACKSON MOSES | UBUNGO | JACKSON MOSES NA LUCIANA JACKSON | KIWANJA | MBEZI MSIGANI | 11/08/2021 NA KUENDELEA |
| | | | | | | |
| 9 | GRACE ELASI MAHUGI | UBUNGO | GRACE ELIAS MAHUGI NA EMMANUEL KASANZU | KIWANJA | MBEZI MALAMBA MAWAILI | 9/08/2021 NA KUENDELEA |
| 10 | WENCESLAUS JOHN MASSAWE | AGGREY | WENCESLAUS JOHN MASSAWE & MATESO JOHN MASSAWE | NYUMBA | MBWENI, TETA STREET | 07/08/2021 NA KUENDELEA |
| 11 | HENRY AUGUSTINO SULUO | ARUSHA | HENRY AUGUSTINO SULUO | KIWANJA | GOMBA ARUSHA | 11/8/2021 NA KUENDELEA |
| 12 | ISIMBULA M RAJABU | ARUSHA | ISIMBULA RAJABU | KIWANJA | ARUSHA | 11/8/2021 NA KUENDELEA |
| 13 | MUNGAYA NDASIKOY | ARUSHA | LEMOMO KORDUNI | SHAMBA | MESERANI ARUSHA | 12/8/2021 NA KUENDELEA |
| 14 | SAING'ORIE KILAMIANI | ARUSHA | SAING'ORIE KILAMIANI | SHAMBA | MESERANI ARUSHA | 12/8/2021 NA KUENDELEA |
| 15 | BABA LEMOMO | ARUSHA | SAING'ORIE KIAMIAN | SHAMBA | MESERANI ARUSHA | 12/8/2021 NA KUENDELEA |
| 16 | SHANI G. WAPALILA | ARUSHA | SHANI G. WAPALILA | NYUMBA | MUSHONO ARUSHA | 13/8/2021 NA KUENDELEA |
| 17 | FATUMA JUMA | ARUSHA | FATUMA JUMA | NYUMBA | NJIRO ARUSHA | 13/8/2021 NA KUENDELEA |
| 18 | FRANK JOSEPH ASENGA | ARUSHA | FRANK ASENGA | NYUMBA | SOMBETINI ARUSHA | 14/8/2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuziatalazimikakulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; **tupigie simu no. 0768672367/ 0785242219 /0784252048/ 0674821287/ 0713604044**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216370902

# Wajawazito walalamikia kusumbuliwa na mifugo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAJAWAZITO ambao wanafika kujifungua katika Zahanati ya Old Shinyanga, wameomba kujengwa uzio katika eneo hilo ili kuwakinga dhidi ya mifugo wanapokuwa wakifanya mazoezi.

Wamesema wakati wakifanya mazoezi, hupishana na mifugo kwa kuwa eneo hilo halina uzio.

Diwani wa Viti Maalum Manispaa ya Shinyanga, Picca Chogelo, alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, uliofanyika Old Shinyanga.

Alisema wajawazito ambao wanafika kujifungua kwenye zahanati hiyo maisha ya yapo hatarini, kutokana na kupishana na mifugo wakati wakifanya mazoezi na kwamba hali hiyo inasababishwa na ukosefu wa uzio na kumwomba Mbunge Katambi awatatulie kero hiyo.

"Mimi kama mama, naomba niwasilishe kilio cha wanawake wenzangu, tunaomba mbunge utusaidie ujenzi wa uzio kwenye zahanati yetu ya hapa Old Shinyanga...wajawazito huwa wanahatarisha maisha yao kwa kupishana na mifugo wakati wakifanya mazoezi," alisema Chogelo.

"Tunaomba pia tujengewe jengo la mama na mtoto kwa ajili ya kujifungua, kinamama wanapata tabu sana wanapofika kupata huduma ya uzazi kwenye zahanati yetu," aliongeza.

Kwa upande wake, Mbunge Katambi, alisema kilio cha kinamama kwenye zahanati hiyo amekisikia, na kuahidi kulifanyia kazi suala hilo la ujenzi wa uzio.

Aidha, alisema atasaidia pia kuongeza idadi ya watumishi wa afya kwenye zahanati hiyo, pamoja na upatikanaji wa dawa za kutosha, ili kuwaboreshea wananchi huduma za matibabu.




Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, Khadija Nassir Ally (katikati), akiangalia viti na meza 50, baada ya kukabidhiwa na Benki ya NMB, kwa ajili ya Shule ya Sekondari Mkugilo pamoja na madawati 62 kwa ajili ya Shule ya Msingi, Chatembo iliyopo Mwandege, wakati wa hafla iliyofanyika jana. Kushoto ni Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mkuranga, Peter Msaki (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mkuranga, Mshamu Munde. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maonyesho ya madini kuipa fursa Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ana tarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye maonyesho ya biashara ya teknolojia ya madini mkoani Shinyanga.

Maonyesho hayo yatafanyika kuanzia leo hadi Agosti Mosi, katika viwanja vya Butulwa, Kata ya Old Shinyanga.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alibainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari.

Alisema maonyesho hayo ni ya awamu ya pili ambayo yamelenga kukuza sekta ya madini, na biashara mkoani humo.

Alisema Mkoa wa Shinyanga una migodi mingi ya madini, hivyo maonyesho hayo yatatoa fursa kwa wawekezaji kuwekeza mkoani humo, pamoja na kuunganisha mtandao wa wafanyabiashara.

"Maonyesho haya ya biashara na teknolojia ya madini mkoani Shinyanga, yatatusaidia kukuza uchumi wa mkoa wetu, na pato la mtu mmoja mmoja, na Taifa kwa ujumla.

"Tunaomba wananchi wajitokeze kwa wingi kwenye maonyesho haya, kuja kuona madini live, pamoja na wafanyabiashara wajumuike ili wapate mtandao na kukuza biashara zao," aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa maonyesho hayo, Kulwa Meshack, ambaye ni Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), mkoani Shinyanga, alisema maonyesho hayo ni fursa kwa wachimbaji na wafanyabiashara, watabadilishana uzoefu namna ya kufanya kazi zao.

# Mradi ulivyosaidia wakazi Dar kuikabili malaria

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Mtaa wa Mwembemadafu Kata ya Ukonga, Wilaya ya Ilala Dar es Salaam wamenufaishwa na mradi maalum wa kupambana na maambukizi ya malaria.

Mradi huo unahusisha kuboresha makazi yao kwa kuweka vyandarua maalum kwenye madirisha ya nyumba ili kuzuia mbu kuingia.

Mradi huo unaotekelezwa kwa ushirikano na Club ya Rotary ya Oysterbay Dar es Salaam, Ukonga, GT Bank na wadau wengine unalenga kusaidia juhudi za serikali za kupambana na malaria kupitia mbinu mbalimbali.

Akizungumza baada ya kutembelea nyumba zaidi ya 30 zilizowekewa vyandarua hivyo maalum za kuzuia mbu, Rais wa Rotary Club ya Oysterbay, Aisha Skyes, alisema mradi huo utasaidia kwa kiwango kikubwa kupuuza maambukizi ya malaria kwenye kata hiyo hasa kwa wanachni wenye kipato cha chini, ambao hushindwa kuboresha makazi yao.


"Utafiti mbalimbali umethibitisha kuwa uwekazi wa neti maalum katika madirisha na milango ya nyumba husaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza maambukizi ya malaria, kwani mbu hushindwa kuingia katika ndani kutokana na uzio huo," alisema.

Kwa mujibu wa rais huyo, kama nchi ikiamua na kutekeleza mradi kama huo, hasa kwenye makazi holela, itasaidia kuwalinda Watanzania dhidi ya ugonjwa huu hatari.

Jacton Ochieng' kutoka Club ya Ukonga, alisema pamoja na kuboresha makazi hayo, mradi huo pia umejikita katika kutoa elimu kwa wakazi wa Ukonga jinsi ya kupambana na ugonjwa huo sambamba na kutoa huduma za vipimo na matibabu bure.

Naye Bendera Ramadhani, diwani wa kata hiyo, alipongeza club za Rotary na wadau wote waliojitoa kusaidia wakazi hao kwa kuboresha makazi yao, hivyo kuwafanya wawe salama.

"Ukizingatia kuwa serikali imekuwa ikiwekeza juhudi nyingi ili kupambana na magonjwa mbalimbali ikiwamo malaria, kuja kwa mradi huu ni neema kwa kata yetu, kwani wakazi wengi wamenufaika na wengine wataendelea kunufaika," alisema.




Viongozi mkiaminiwa, pia mjiamini

Ukurasa 13



Ukurasa 14

**Kijana aliyeshangaza kuacha kazi ghafla, kajiajiri na kuajiri saba, lengo wafike 50**


# BUFE
Ijumaa JULAI 23, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


UCHUMI

# PASS TRUST
## Wabia serikalini 'PPP' walioweka kambi Dodoma 2021 kueneza Kilimo Biashara

- Nusu wanufaika kinamama; ajira milioni 2.5
- Miradi 46,300 na wajasiriamali milioni 1.7

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KITAIFA kuanzia sera hadi falsafa 'Kilimo ni Uti wa Mgongo.' Ndio imeushika uchumi wa taifa. Utekelezaji wake unagusa mtazamo wa sura mbili, ubia katika serikali na sekta binafsi, kupitia sheria maalum inayojulikana kwa kifupi PPP (Ubia wa Sekta Binafsi na Umma).

Hapo katika mlango wa sekta binafsi, ndipo inapopatikana taasisi ya Pass Trust iliyojikita katika utekelezaji kilimo nchini, kusaidia kuwainua wajasiriamali wa sekta ya kilimo, mtazamo uwe wa kibiashara.

Pass Trust, ilianzishwa kwa ushirikiano wa serikali za Tanzania na Dermark miaka 20 iliyopita, lengo ni kuwezesha upatikanaji huduma za kifedha na biashara kwa bidhaa na huduma katika sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi nchini

Dhima kuu ilijikita katika kupunguza umaskini, huku ikiwezesha upatikanaji mitaji kwa wakulima, yenyewe ikijikita jukumu la udhamini.

Imekuwa ikiwezesha mikopo wastani wa asilimia 20 hadi 80 kwa wanawake, ikiwa ni njia ya kuongeza dhamana ya kuwawezesha wateja kupata mikopo hiyo na katika hilo, Pass hadi sasa inafanya kazi na benki 14 zilizopo nchini kwa mkataba maalum.

Pia, asasi hiyo inatoa huduma za ukuaji biashara kama vile mafunzo ya ujasiriamali, upembuzi yakinifu wa miradi husika, unaosaidia wateja kuandaa maandiko ya miradi bora ya uwekezaji.

Mikakati iliyopo ni kwa taasisi inalenga kusaidia sekta ya kilimo kuwasaidia wajasiriamali, kuwainua kiuchumi kwa kuwapatia mikopo



Moja ya shughuli za maonyesho ya kilimo yaliyofanywa na PASS Trust. **PICHA: MTANDAO.**

ya pembejeo, zana za kilimo na ufugaji na zinazosaidia kuendesha ujasiriamali.

Hadi sasa PASS imeshadhamini miradi ya wajasirimiali 46,300, huku kuna wajasiriamali million 1.7 wanaonufaika na udhamini huo, pia fursa za ajira.

**MKURUGENZI PASS**

Anna Shanalingigwa, ni Kaimu Mkurugenzi wa asasi ya PASS, anasema ilianzishwa mwaka 2000 na hadi sasa imeshadhamini miradi 46,300 wenye thamani ya Sh. trilioni moja na kuna wajasiriamali milioni 1.7 waliokwishanufaika na udhamini huo.

Mkurugenzi huyo anasema, asilimia 45 ya wanufaika hadi sasa ni wanawake, pia ajira sasa imefika watumishi milioni 2.5.

Kwa nini jijini Dodoma?

Anna anaimbia Nipashe kwamba wako katika mzunguko wa kutoa huduma ya kilimo na upatikanaji fedha za kuchochea ukuaji wa kilimo biashara nchini na wameandaa maadhimsho yaitwayo 'Wiki ya PASS'.

Ni tukio linalowaleta pamoja wakulima wauzaji zana za kilimo, pembejeo, taasisi za fedha, viongozi wa serikali na wachakataji, wakutane kujadili kupatikana fedha za kuchochea ukuaji kilimo biashara.

Pia, anamtaka kuwapo kampuni ya PASS Leasing inayojihusisha na mikopo ya kilimo bila ya dhamana kwa wakulima ngazi zote: Wadogo, kati, wakubwa na vikundi mbalimbali, lengo ni kukuza mnyonyoro wa thamani ndani ya kilimo.

**DC DODOMA**

Jabir Shekimweri, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, akizungumzia katika Wiki ya PASS Trust inayofanyika katika viwanja vya Nyerere Sguare, anasema asasi PASS Trust ina fursa ya kuwekeza katika zao la zabibu, yenye faida kubwa.

Rai yake Shekimweri ni kwamba, ufike wakati wakulima wafanye kilimo chenye tija, kwani mwelekeo uliopo sasa ni jamii kujikita zaidi katika kilimo biashara, hivyo anasogeze wito hadi kwa wafugaji, wavuvi na wajasiriamali katika mnyonyoro wa thamani wa kilimo

**WAKULIMA NA YAO**

Mkulima Japhet Lusita, anaeleza matarajio yake kwamba taasisi hiyo itasaidia hasa katika miongozo, hasa ya kutoa mikopo ya zana za kilimo, akiamini ni moja ya maeneo yatakayowasaidia kwa kiasi kikubwa wakulima kuinuka na kusonga zaidi katika dhima wanayoielekeza, kilimo biashara.

Sura tofauti ya matarajio ni kunufaika na mikopo. Anaongeza:"Hii itatusaidia wakulima wengi kupata fursa nyingi kutoka katika taasisi hiyo na wataalamu wa sekta ya kilimo ambao watakuwapo."

Lusita anafafanua kwamba, maadhimisho hayo yaliyofanyika Nyerere Square, ni fursa yao kukutanisha wakulima kutoka maeneo mbalimbali, kwa ajili ya kuwaelekeza namna fursa za kilimo zilivyo.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba.

## RC MGUMBA:

# Nimekuja na mpango mkakati kulinda mipaka ya nchi Songwe ing'are

- Ajigamba ya tatu kulisha nchi, ataendeleza
- Mpakani Tunduma nako kunapaishwa upya
- Autaja ni mkoa mchanga, ila mambo yake ...

**Na Nebart Msokwa, SONGWE**

AKIWA anahesabu miezi tangu alipoteuliwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, ameweka bayana vipaumbele vyake katika utendaji kazi ndani ya mkoa huo.

Hapo kipaumbele chake, kinaangazia kulinda usalama wa wananchi, mali na mipaka ya nchi. Mgumba anaiambia Nipashe kwamba mkoa huo ni mchanga kuliko mingine yote nchini na unapakana na nchi mbili za Zambia na Malawi, hivyo ulinzi kwenye mipaka yake muhimu kwa usalama wa nchi.

Hapo katika nafasi yao pekee, unatajwa mpaka wa Tunduma, kati ya Tanzania na Zambia ambao ni nyenzo nyeti katika uchumi wa nchi kihistoria.

Anataja kipaumbele chake cha pili ni kuimarisha sekta ya kilimo kwa lengo la kuinua kipato cha wananchi wa mkoa huo na kuhakikisha kunakuwapo usalama wa chakula mkoani humo na hata kwa taifa zima.

Anasema Songwe, ni mkoa wa tatu kitaifa kwa uzalishaji mkubwa wa zao kahawa, nyuma ya Kilimanjaro na Kagera.

Katika hilo, anataja dhamira yake inasimamia kuhakikisha kilimo cha zao hilo, pamoja na mazao mengine ya kibiashara kwa ajili ya uchumi wa wananchi.

"Pia Mkoa huu ni wa tatu kitaifa kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, hususani mahindi. Kwa hiyo, hiki ni kikapu cha taifa, tunategemewa kwa ajili ya kulisha taifa hili, lazima tusimamie kilimo ili tujilishe sisi wenyewe na tulishe na watu wengine," anasema Mgumba.

Anaendelea: "Mkoa wetu pia unapozungumzia Songwe unazungumzia uvuvi maana tuna Ziwa Rukwa, ambalo lipo ndani ya mipaka yetu. Tutahakikisha tunasimamia uboreshaji wa sekta ya uvuvi, ili iwaingizie kipato wananchi wetu."

Vilevile, Songwe imo katika mikoa ambayo wananchi wake ni wafugaji na anasisitiza kwamba, atasimamia wananchi wake wanaachana na ufugaji wa asili na kuhamia ufugaji wa kisasa, hata ukaongeza tija kimkoa.

Mgumba ambaye kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2020, alikuwa Naibu Waziri wa Kilimo, anasema mkoa anaouongoza una maeneo mengi yanayofaa kwa ufugaji nyuki, hasa katika misitu iliyoko wilayani Songwe, hivyo analenga kusimamia na kuimarisha sekta, ili iwasaidie wananchi kuongeza kipato.

Ahadi yake ni kuhakikisha kwamba, atasimamia vyema sekta hizo na kuzisaidia kuimarisha lishe, kwa wananchi, ili kukabiliana na tatizo la udumavu ambalo linakabili sehemu ya jamii.

**SEKTA MADINI**

Mgumba anasema kipaumbele chake ni kusimamia sekta ya madini, ili kuhakikisha inawanufaisha wananchi wa mkoa huo na taifa, kwa maelezo kuwa sekta hiyo ni muhimu na miongoni mwa shughuli zinazoziingizia taifa fedha nyingi.

Hapo anawapa moyo wachimbaji wadogo wa madini, kwa kuwahakikisha anawalinda na kuwagawia maeneo ya uchimbaji, ili wayamiliki na kufanya kazi zao kwa uhuru.

"Tunataka wachimbe, wauze, wajiongezee kipato na walipe kodi kwa ajili ya maendeleo ya taifa, madini haya ni kwa ajili ya taifa zima.

"Lakini nawakazania zaidi wananchi wa Songwe kwa sababu mkoa huu ni kitindamimba kimuundo na tunatakiwa tuujenge," anasema Mgumba.

Mkuu wa Mkoa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anawataka wachimbaji wadogo wachangamkie fursa ili wanufaike na sekta hiyo, kwa maelezo neema imeshaanza kufunguka.

**UBORESHAJI BIASHARA**

Mkuu wa Mkoa Mgumba, anasema katika mkoa huo mchanga, biashara ni miongoni mwa shughuli zao kuu za kiuchumi, zinazofanyika na zinahitaji usimamizi wa karibu.

Ahadi yake ni kuhakikisha kwamba, anasimamia kwa umakini shughuli na hasa mpakani katika mji wa Tunduma, ambao wakazi wake wengi shughuli yao kuu ni biashara, pia kutokana na kukosa nyingine kutokana na uhalisia wa vikwazo mazingira.

"Wakazi wa Tunduma hawalimi, hawafugi, hawachimbi madini na wala hawavui samaki, shughuli zao ni biashara, tutahakikisha tunawawekea mazingira mazuri ya biashara ili wapate faida, wakuze mitaji yao na walipe kodi ya serikali," anasema Mgumba.

Mkuu wa Mkoa anapaza sauti kwa wafanyabiashara wanaotaka kwenda mkoa humo, kwamba amejipanga anawasaidie ufanisi upatikane, katika mazingira ya utulivu.

FURSA UWEKEZAJI

Mgumba ambaye kitaaluma ni mtaalamu wa usimamizi wa biashara, anasema mkoa wa Songwe una fursa mbalimbali za uwekezaji, ikiwamo kwenye sekta za kilimo, uvuvi, madini na biashara na kwamba kila moja ina eneo maalumu linalofaa shughuli hizo.

Anafafanua, kuwapo fursa za uwekezaji kwenye viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali, ukiwamo mpunga unaolimwa katika Bonde la Kamsamba wilayani Momba, mahindi pamoja na mazao mengine.

Mkuu wa Mkoa anasisitiza: "Vipaumbele vyote nilivyovitaja ni fursa kwa wawekezaji kutoka katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kuja mkoani kwetu kuwekeza na sisi kama serikali tutaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji kuja kuwekeza."

Anasema kuna vipaumbele vilivyoainishwakwa kushirikiana na sekta binafsi katika kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo, hivyo atahakikisha wawekezaji wanaandaliwa maeneo ya kuwekeza.

**SHIDA YAKE**

Mgumba anasema, mkoa wake wenye wilaya nne na halmashauri tano, unakabiliwa na tatizo la kukatika kwa nishati ya umeme, hali inayowakatisha tamaa baadhi ya wawekezaji.

Anasema tatizo hilo linasababishwa na mkoa huo kuendelea kutumia njia moja pamoja na Mkoa mama wa Mbeya hali inayosababisha umeme ukikatika Mbeya lazima ukatike na maeneo yote ya mkoa wake.

Anafafanua kwamba, hivi sasa tayari wanaendelea na ujenzi wa njia mpya ya umeme kutoka jijini Mbeya ambayo itatenganishwa na ile inayotumika Mbeya ili kusiwapo na uhusiano wa moja kwa moja kati ya njia hizo.

Mgumba anasema ujenzi wa njia hiyo baada ya kukamilisha, watagawa tena njia hizo ili kila wilaya ya mkoa huo iwe na njia yake jambo ambalo litasaufanya nishati hiyo ikikatika kwenye wilaya moja nyingine iendelee kupata.

"Lakini, tutaendelea kusambaza umeme kwenye vijiji vyote vya mkoa wetu kupitia mradi wa REA, ili sasa tuvutie wawekezaji wa viwanda, tunataka watu waweke viwanda vya kuchaka mazao mpaka vijijini.

"Tunataka tuache kusafirisha mpunga kutoka Kamsamba na badala yake watu wajenge viwanda vya kuchakata mpunga mpaka Kamsamba ili tuache kusafirisha mazao ghafi," anasema Mgumba.

Anaahidi atahakikisha anaendeleza mema yote yaliyoanzishwa na watangulizi wake ambao ni Luteni Mstaafu Chiku Galawa na Brigedia Jenerali Nicodemas Mwangela.






Mandhari ya mji wa biashara Tunduma na mpaka wake, unaotenganisha Tanzania na Zambia, ambao ni sehemu ya kitovu cha uchumi wa mkoa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Viongozi mkiaminiwa, pia mjiamini




**Na Joseph Kulangwa**

WAZAZI hujivunia sana wanapopata watoto na huwa ni shangwe zaidi anapokuwa ni mtoto wa kwanza kuzaliwa katika ndoa mpya. Ndiyo sababu, wazazi wanapoozesha hutamani sana kuona zao la kwanza la wanandoa.

Hivyo, mtoto anapozaliwa 'huengwaengwa' na kutunzwa kila inavyowezekana, ili akue na afya njema, kwa kuwa anakuwa pengine hana pa kutegemea zaidi ya wazazi wake, ambao kwa kweli ndio miungu wake duniani.

Kila anapokua, wazazi hufuatilia ukuaji wake, atakaa, atatambaa, atasimama hatimaye atakimbia, huku pia kama hana tatizo lolote atazungumza na kuwasiliana na wazazi wake. Muda wote huo kabla ya kuanza na anapoanza shule, bado anakuwa tegemezi.

Wazazi wanakuwa wanajua fika, kwamba hawezi kujitegemea, hawezi kufanya lolote bila msaada wa wazazi. Atasoma, akue kiume, wazazi watatambua lakini ataendelea na shule hadi amalize anapostahili kumalizia.

Akishamaliza shule ametimia kike au kiume, anaweza kuhama nyumbani kwa wazazi na kwenda kujitegemea kwa kila kitu, ikiwamo pia kujitegemea kwa mawazo, kwamba anaweza sasa kujiamulia lipi baya na zuri.

Hapo ndipo sasa mzazi anakuwa na uhuru wa kumpa mwanawe majukumu yakiwamo ya kufanya mambo hata kwa niaba yake, hivyo mtoto kuwa na



NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

ujasiri wa kuamua mambo anayoyataka mzazi wake kwa sababu anakuwa tayari ameshamwelewa.

Wapo wazazi ambao wanaweza kufuatwa na watu kwa ajili ya msaada fulani hata kama si wa mali, wa hali na mzazi akaagiza mwanawe amalize tatizo hilo, kwa sababu anamwamini na ndiyo sababu ya kumpa majukumu hayo.

Hii ni sawa na uongozi, kwamba kiongozi anapopewa majukumu na mkuu wake, ina maana amemwamini kwamba anaweza kutekeleza kwa kiwango ambacho mteuzi amemwamini kukifanya na kukifikia.

Rais anapoteua mawaziri, wakuu wa mikoa, wa wilaya na wakurugenzi wa mikoa na wilaya au makatibu tawala wa wilaya na mikoa, huwa ameshawaamini kwamba wanaweza kumwakilisha vizuri katika maeneo waliyomo.

Hivyo basi, wateule wanapaswa kumthibitishia mteuzi kwamba wanaweza kutimiza majukumu waliyokabidhiwa kama si kwa asilimia 100, basi angalau asilimia 90 au 80 isipungue hapo, ni dhahiri kuwa hawawezi kutekeleza kwa zaidi ya asilimia 100.

Tanzania pengine na mataifa mengine tusiyoyajua, imeshuhudia mambo mengi yanayofanywa na wateule na kujiuliza kama kweli wanatosha katika maeneo waliyopewa au wapo kujaza nafasi tu.

Mathalan, anaweza kumwamini mtu akampa mkoa, akampa wilaya au eneo la kusimamia ili yeye abaki afanye yale yanayolihusu Taifa ikiwa ni pamoja na uhusiano wa kimataifa, lakini anayepewa anakuwa hawezi kukidhi, bila kukemewa au kufuatiliwa na mteuzi wake.

Tumeshuhudia baadhi ya viongozi, kila akisimama kuzungumzia maendeleo katika eneo lake la uongozi, lazima amtaje wa juu yake kiungozi, kana kwamba anapotaka kitu mahali hapo yupo.

Mathalan, kuanzia kipindi cha tulikotoka na hadi tuliko sasa kwa baadhi tunasikia hawawezi kusema lolote bila ya kutaja majina yake wa juu, ndio nguzo ya hoja zao, wakati wana nafasi ya kufikisha ujumbe bila ya kuegemea kutaja majina hayo ya juu.

Hilo baadhi ya watu wamekuwa wakisema ni kujikomba kusiko na tija, ni kujitetea katika namna ya kutojiamini kama anatosha katika nafasi aliyonayo au ana utaalamu wa kumudu alichopewa kukifanya.

Wapo viongozi wanaopenda kusifiwa, kuimbiwa na kupigiwa makofi, lakini wapo wasiopenda hali hiyo, hasa wanaoamini kwamba katika jamii kuna vinyonga na kuna watu na viatu. Alamsiki!

## UJASIRI WA UWEKEZAJI

# Kijana aliyeshangaza kuacha kazi ghafla, kajiajiri na kuajiri saba, lengo wafike 50

- Sifa yake; alithubutu zama ya corona

**Na Frank Monyo**

RICHARD Steven, kijana wa Kitanzania mwenye umri miaka 30. Kitabia, huwa ana uthubutu na ubunifu unaomuwezesha kutoa ajira kwa vijana saba, huku lengo lake ni angalau kutoa ajira 50,000 itakapotimu mwishoni wa mwaka huu.

Ni namna gani alianza 'kuikokotoa' fursa hiyo, katika kipindi cha mwanzo cha janga la corona, baada ya kubuni njia mbadala ya kuingiza kipato kwa kusafirisha mizigo midogo na mikubwa majumbani kwa wanaotuma na kutumiwa kutoka nje ya jiji la Dar es Salaam na hata nchi, akitumia usafiri wa mabasi.

'Dar Delivery' ndio kampuni husika, ambayo mbali na kusafirisha mizigo, pia inasambaza kadi za harusi, chakula ndani ya Dar es Salaam na nakala za kiofisi kwa kutumia pikipiki.

"Msukumo wa ubunifu wangu ulikuja zaidi baada ya kukutana na changamoto ambayo kwangu nilichukulia kama fursa iliyotokea katika kampuni ambayo nilikuwa naifanyia kazi, ambayo ni kubwa Tanzania na Afrika Mashariki, na hapo nilikuwa nalipwa mshahara mkubwa," anadokeza.

Richard anasema, mwanzoni hapakuwapo mtu aliyemuelewa sababu za kuacha kazi yenye maslahi makubwa, akijielekeza kwenda mtaani na wakati huo mazingira ya jamii kukabiliwa na janga la corona iliyojitokeza wakati huo.

Anasema, baada ya watu wengi kupunguza mizunguko kwa kuhofia maambukizi ya corona kipindi cha maradhi hayo, ndipo wazo jipya lilipozaliwa.

Richard anasimulia: "Nilikuwa na wazo, nikamshirikisha rafiki yangu wa karibu. Tukaamua kuanza kuishi kwenye wazo letu baada ya kuona fursa ni kubwa wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona, wananchi walipopunguza mizunguko na kukaa nyumbani (Lockdown).

"Wakati wa corona, watu walishindwa kutoka majumbani hapo ndipo lilikuja wazo la kuleta huduma ya 'delivery' (usambazaji). Baada ya majadiliano, tukaja na jina la Dar Delivery.

"Pia, tulifanya utafiti na kugundua kuwa mbali na 'lockdown' (vizuizi nyumbani), Dar es Salaam watu wengi wapo 'busy' (wametingwa) sana, tukasema huduma pekee tunayoweza kuwarahisishia ni suala zima la muda.

"Kwa hiyo, sisi 'Dar Delivery' tunatoa huduma mbalimbali, yaani mtu anaweza kutuagiza bidhaa yeye akaendelea na majukumu yake, sisi tukamletea hadi alipo," anasema Steven

### AJIRA ILIVYO

Anasema kwa sasa kampuni hiyo ina wafanyakazi saba ambao kila mmoja amekabidhiwa pikipiki yake na kwa mwezi wanatumia zaidi ya Sh. milioni 2.3 kulipa mishahara ya vijana hao.

"Tulivyoanza tofauti na sasa. Awali tulikuwa tunakodisha pikipiki kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya wateja wetu, lakini kwa sasa tunamiliki pikipiki ambazo vijana wetu wanazitumia kutoa huduma kwa wateja ndani ya Dar es Salaam," anasema.

Anaongeza: "Mpaka sasa ukiachilia matumizi mengine, mishahara kwa wafanyakazi wa 'Dar Delivery' ni zaidi ya milioni 2.3, jambo ambalo tunajivunia kuweza kutoa ajira kwa vijana wenzetu," anasimulia



Mizigo ikiwa ofisini, Sinza, Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: FRANK MONYO**

> **Tulivyoanza tofauti na sasa. Awali tulikuwa tunakodisha pikipiki kwa ajili ya kusafirisha mizigo ya wateja wetu, lakini kwa sasa tunamiliki pikipiki ambazo vijana wetu wanazitumia kutoa huduma kwa wateja ndani ya Dar es Salaam**

### SAFARI INAKOELEKEA

"Dar Delivery itafika mbali sana, kwani malengo yetu ni makubwa sana. Tunatamani kutoa ajira zaidi ya 50,000 kwa vijana hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu. Tuna mpango wa kumiliki ofisi yetu kubwa, kuwa na 'Apps' (Applications) ya 'Dar Delivery' ambayo itamsaidia mteja wetu kutuagiza mizigo yake wakati wowote," anasema Steven

Anasema gharama za kusafirisha mizigo zinategemeana na umbali ambao mteja yupo, ingawa anasema walichozingatia ni kuweka gharama ndogo ambazo hazitamuumiza mteja.

"Lengo letu ni kuwarahisishia watu kwenye hii huduma hasa suala zima la muda na ndio maana hata gharama zetu sio kubwa.

"Mfano, kuchukua mzigo mdogo Shekilango (Sinza - Dar es Salaam) kwenda Kariakoo ni Sh.4, 000 tu na hizi bei mara nyingi inategemea umbali na aina ya mzigo, mfano kuchukua simu Kariakoo hadi Mbezi Beach ni Sh. 5,000 tu," anaeleza.

### USAMBAZAJI KADI

Richard anasema huduma ya kusambaza kadi za harusi imetokea kupendwa na watu wengi, kwani ina tija kwa mahitaji yao.

"Unajua kwenye vikao vya mwisho vya harusi, changamoto kubwa ni watu kufika na kukabidhiwa kadi ya ukaribisho wa sherehe ya harusi. Sisi kazi yetu ni kuomba kazi hiyo ya kutumwa kusambaza, wanatupa namba ya simu ya mhusika na mahali alipo, sisi tunazifikisha kwa gharama nafuu," anasema

Msisitizo wake ni kwamba gharama za usambazaji kadi za harusi inategemea na idadi ya kadi na umbali wa eneo ambako inatakiwa kufikishwa ndani ya Dar es Salaam.

"Gharama huwa inategemea na idadi ya kadi, kwa hiyo kadi zikiwa nyingi gharama inapungua zaidi, ila zikiwa chache gharama inakuwa ya kawaida. Mfano mtu akiwa na kadi 200, tunasambaza kila kadi moja kwa Sh. 500 tu na hicho ni kiwango ambacho tunapendelea kusambaza," Richard anaeleza.

Msisitizo wake ni kwamba kwa sasa wana mtandao mkubwa na washereheshaji ambao huwa wanawasiliana nao na kuwapa kazi, pamoja na kutembelea vikao vya harusi kwa lengo la kuomba kazi hiyo ya usambazaji.




Msafirishaji mizigo kwa njia ya pikipiki akiwa kazini.



# RC alia udumavu Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wataalamu wa lishe kuboresha hali ya lishe mkoani humo ili kupunguza udumavu.

Mtaka aliagiza hayo jana baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2021 ambayo inaonyesha Dodoma ina watoto wenye udumavu kwa asilimia 37.2, ukondefu asilimia 3.7 na upungufu wa uzito asilimia 17.8.

Alisema hali hiyo inapaswa kutazamwa kwa umakini kwa kuwa vyakula vipo lakini elimu ya namna ya uandaaji wa lishe kwa watoto ni tatizo kwa wazazi hususani wa maeneo ya vijijini.

"Inasikitisha kuona udumavu kitaifa upo asilimia 31.8, huku Dodoma ikiwa na asilimia nyingi kuliko kitaifa.

"Tunapaswa kuweka jitihada za kuondokana na udumavu, ukondefu na upungufu wa uzito. Wataalamu wa lishe mpo, fanyeni kazi ya kutoa elimu ili jamii ielimike kwenye suala zima la lishe kwa watoto," aliagiza.

Mtaka alisema mkoa umeendelea kusimamia upangaji na kutenga fedha za kutekeleza afua za lishe, kuboresha uibuaji na matibabu ya utapiamlo mkali pamoja na kuongeza juhudi za utoaji wa unasihi wa lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma za afya.

Awali, akisoma taarifa ya utekelezaji wa viashiria vya mkataba wa lishe, Ofisa Lishe wa Mkoa wa Dodoma, Herieth Careen, alisema fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za lishe kwa kipindi cha Aprili hadi Juni ni Sh. milioni 166.9 ambazo zimetumika sawa na asilimia 104.7.

Alisema matibabu ya watoto wenye utapiamlo mkali hutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya na katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2021 watoto 880 waliibuliwa ambapo kati yao, 773 walipatiwa matibabu. Alisema hatua hiyo ni nzuri na inaonyesha jitihada zinazofanywa na wataalamu wa lishe kuhakikisha wanatokomeza utapiamlo kwa watoto wadogo.

"Utoaji unasihi juu ya ulishaji wa watoto wachanga na wadogo kutoka kwa watoa huduma kwa afya ngazi ya jamii kwa kipindi cha robo ya nne, jumla ya kinamama/walezi 46,060 kati ya 49,568 walio na watoto wa miezi 6-23 walipatiwa unasihi juu ya ulishaji lishe kwa watoto," alisema.

Alisema utoaji nasihi uliofanyika kwa kinamama hao ni pamoja na ulishaji vyakula vya nyongeza kwa wazazi walezi wenye watoto wa umri wa miezi 6-23.

Ofisa huyo alisema jitihada za kuwapatia elimu kinamama wenye watoto juu ya utoaji lishe kwa watoto hao zinafanyika, lengo likiwa kutokomeza utapiamlo na upungufu wa uzito kwa watoto wadogo.

## Serikali yasikiliza kilio cha wananchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesikia kilio cha wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini kujengewa barabara ya lami kuanzia njia panda ya Chamwino Ikulu hadi Mvumi Makulu yenye urefu wa kilomita 75.

Wananchi hao kwa muda mrefu wamekuwa wakipaza sauti kuomba kujengewa barabara hiyo ili kuondokana na adha iliyokuwa ikiwakabili hususan wakati wa msimu wa mvua.

Akizungumza na wanachi wa Kikombo juzi alipokuwa akitoa shukrani na kusikiliza kero za wananchi, Mbunge wa Jimbo hilo, Anthony Mavunde, alisema serikali imesikia kilio cha wananchi.

Alibainisha kuwa mwaka huu, ujenzi utaanza kwa kilomita 16.8 kutoka njiapanda ya Chamwino Ikulu kuingia ndani Kikombo na kutoka Ntyuka hadi Chidaya.

Mavunde alisema zabuni ya kumpata mkandarasi ambaye atajenga barabara hiyo na madaraja makubwa itatangazwa mwezi ujao.

Alibainisha wakazi wa Kikombo wanakabiliwa na kero ya muda mrefu hasa wakati wa mvua ambapo vivuko hujaa maji na hulazimika kupitia njia ya Ihumwa.

"Pia, Ihumwa mbele barabara haikuwa nzuri, baada ya serikali kuelekeza Makao Mkuu ya Jeshi kuwa Kikombo, mimi kupitia Bunge na mbele ya Hayati Magufuli tulimwomba maana barabara hii ina urefu wa kilomita 75 inaunganisha Mvumi hadi Ntyuka, tuliomba ijengwe kwa kiwango cha lami,"alisema.

Mbunge huyo alisema ujenzi wa barabara hiyo utasaidia kurahisisha usafiri kwa wananchi wanaokwenda hospitali ya macho Mvumi na Hospitali ya Ntyuka.

Kuhusu mradi wa maji Chololo, Mavunde alisema fedha zimepatikana na mwaka huu kitachimbwa kisima kipya wakati wakiendelea na mradi wa Kikombo na ukarabati wa miundombinu.



Meneja wa kampuni ya Zana za Kilimo Ltd, Hassan Hassan (kulia), akitoa maelezo kuhusu matumizi ya trekta aina ya kubota kwa Matiku Maseke, wakati wa maonyesho ya zana za kilimo yanayoendelea kwenye viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. Trekta hilo, linauzwa Sh. milioni 9.5. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## TARI yapewa kazi kilimo cha zabibu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimwer, ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) kushirikiana na Taasisi ya PASS Trust inayojihusisha na masuala ya kilimo ili kuendeleza kilimo cha zabibu jijini Dodoma.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, Shekimweri, alisema TARI na PASS wanapaswa kutoa mafunzo zaidi kwa wataalamu watakaobobea kwenye kilimo cha zabibu ili kuleta tija katika kilimo hicho.

Alisema taasisi hizo zinapaswa kutengeneza wataalamu kwa ajili kuinua kilimo hicho kiwe na tija.

Shekimweri alisema serikali imeweka mkazo katika suala la kilimo hususani katika zao la zabibu, hivyo TARI wanapaswa kushirikiana na Pass Trust katika kuhakikisha wanasaidiana kuinua sekta ya kilimo mkoani Dodoma.

"Hivi karibuni Waziri Mkuu alisisitiza zao la zabibu litiliwe mkazo, hivyo nao wanapaswa kushikana na PASS Trust kuinua kilimo cha zabibu mkoani hapa,"alisema Shekimweri.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Trust Pass, Anna Shanalingigwa, alisema asasi hiyo imedhamini miradi 46,300 huku wajasiriamali milioni 1.7 wakinufaika na udhamini huo.

Alisema wanufaika ni kutoka sekta ndogo za mifugo, uzalishaji wa mazao, viwanda vya usindikaji, biashara ya mazao, mitambo ya mashine za viwanda, miundombinu bora ya umwagiliaji, usafirishaji wa mazao ya kilimo, ufugaji nyuki, ufugaji samaki na biashara ya pembejeo.

Kaimu Mkurugenzi huyo alisema lengo lao ni kuona wajasiriamali wanafanya ujasiriamali wenye tija kupitia taasisi ya PASS Trust.

Alisema asasi hiyo itawawezesha wakulima wadogo wa kati na wakubwa ikiwamo vikundi vinavyojihusisha na shughuli za kilimo katika mnyonyoro mzima wa thamani kunufaika na zana ambazo zitatolewa kwa mkopo.

Alisema wajasiriamali wanapaswa kujitokeza kwa wingi katika wiki ya PASS ambayo ilianza jana hadi Julai 24 jijini hapa.



# Shule zanufaika madawati kutoka TFS

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania, (TFS) imetoa madawati 200 yenye thamani ya Sh. milioni 15 kwa ajili ya shule sita za msingi zilizoko katika Wilaya za Rungwe na Mbeya.

Mhifadhi Mkuu wa Msitu wa Kiwira wilayani Rungwe, Lucas Sabida, alikabidhi madawati hayo jana kwa Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, kwa lengo la kutatua uhaba wa madawati kwa wanafunzi 600 wa shule hizo.

Alisema mbali na kuchangia madawati, kila mwaka wanatoa miche 70,000 kwa jamii ili kuhamasisha utunzaji mazingira katika maeneo ya hifadhi ya msitu wa Kiwira.

"Kama taasisi ya serikali pia tunachangia katika shughuli za miradi ya maendeleo sambamba na elimu, afya, zaidi ya Sh. milioni 3.4 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya," alisema Sabida. Dk. Anney aliwaonya wananchi kujihusisha na uchomaji moto na kwamba serikali haitawafumbia macho na itawasaka popote walipo.

Alisema wako watu wanajifanya wana vichaa wanateketeza moto misitu pasipo kujua ni mali yao na serikali na kwamba ufike wakati kwa jamii kutunza rasilimali hizo ili baadaye ziwatunze.

"Sitapenda kusikia watu wanachoma msitu huu kwani hapo awali inasemekana kila siku ulikuwa ukichomwa moto. Sasa imetosha na nitakuja kufanya msako wa kimya kimya na watakaobainika, hususan wanaotorosha mbao kwa njia zisizo halali kwa kukwepa kulipa ushuru," alisema.

Diwani Igoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Andrew Mwaipopo, alisema uwapo wa shamba hilo umekuwa mkombozi katika kuchangia miradi ya maendeleo na pia walipokea zaidi ya Sh. milioni 3.4 kwa ajili ya ujenzi Kituo cha Afya cha Ilingi.

Mwaipopo uwapo wa TFS umekuwa mkombozi kwao kwa kuwa inashiriki shughuli zote za maendeleo ikiwamo ujenzi vituo vya afya, miundombinu ya barabara na madarasa pamoja na madawati.



Mwakilishi wa kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Anwar Zaidy (kulia), akikabidhi boksi lenye vifaa tiba kwa Mwenyekiti wa Bodi ya afya ya Halmashauri ya Mji wa Masasi, mkoani Mtwara, Issa Makwelanga (wa pili kushoto), uliotolewa kupitia taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation kwa ajili ya watoto njiti katika Hospitali ya Mkomaindo, wilayani humo. Kushoto ni Mganga Mkuu wa halmashauri hiyo, Dk. Salum Gembe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zimamoto yatoa elimu ya majanga

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya, limeanzisha mpango wa kuwafikia wafanyabiashara katika masoko na kutoa elimu ya kukabiliana na majanga ya moto.

Mbali na kuanza kwa utaratibu huo, pia limeiomba serikali kuangalia mifumo mizuri ya ujenzi wa masoko ili kuondokana na majanga hayo.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, Ofisa Habari Msaidizi wa zimamoto Mkoa, Konstebo Ester Kinyanga, alisema wameona ni vyema kuwafikia wafanyabiashara katika masoko ili wachukue tahadhari mapema.

"Kuna tatizo kubwa kwenye mifumo ya ujenzi wa masoko hususani miundombinu ya barabara sambamba na ujenzi holela wa vibanda vya biashara hususan mama lishe," alisema.

Alisema pia serikali iko katika mpango wa kuboresha vikosi vya zimamoto na uokoaji nchini kwa kupeleka vitendea kazi husUsan magari na kwamba kwa Jiji la Mbeya kuna magari mawili na moja kati ya hao liko kwenye matengenezo.

Naye mtaalam mbobezi wa masuala ya mipango miji mkoani Mbeya, Prince Mwaihojo, alisema halmashauri ya jiji itekeleze mpango wa kuhamasisha wananchi kujenga kwa kufuata ramani zinazotolewa na ofisi za mipango miji ikiwamo ujenzi wa masoko ili kuupendezesha mji lakini pia kuupa urahisi kukabiliana majanga ya moto pindi yanapotokea.

"Miongoni mwa vikwazo vinavyodidimiza Mkoa wa Mbeya na kuufanya kuwa na mpangilio mbovu wa majengo ni siasa za ovyo. Ni wakati sasa kila mwana Mbeya kutanguliza uzalendo kwanza wa kupiga hatua za kiuchumi kwa kuwezesha miradi ya masoko kuwa katika hali nzuri hususani miundombinu ya mabanda, maji na barabara," alisema Mwaihojo.

# Wakulima wa mpunga wajazwa mamilioni

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAKULIMA wa Mpunga Mbarali mkoani Mbeya, wamenufaika na ruzuku ya Sh. milioni 470 kwa ajili ya kuongeza tija ya uzalishaji na ubora wa zao hilo hususani matumizi ya teknolojia za kisasa na kupata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.

Mkulima Andrew Mwambengeo kutoka Kijiji cha Mswisi, ambaye amenufaika na ruzuku hiyo kupitia kampuni ya Azimio Mswisi kwa ufadhili ya shirika la Marekani la USADF, alisema fedha hiyo imefika kwa wakati, hivyo italeta matokeo mazuri kwa msimu huu wa kilimo.

Alisema jitihada hizo za kuwezeshwa fedha kwa ajili ya kuboresha kilimo cha mpunga zinatokana na uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na mataifa mengine ambayo yamekuwa yakishawishiwa kuwekeza nchini ili kuisaidia serikali kuwakwamua wananchi dhidi ya umasikini.

Mkulima mwingine, Batsanje Fumbo, alisema ruzuku hiyo itawanufaisha wakulima wanachama na wasio wanachama wa Azimio Mswisi, kampuni inayojihusisha na uzalishaji wa mpunga na uboreshaji wa mchele.

Katibu wa Kampuni ya Azimio, Lukman Shirima, alisema shirika hilo la Kimarekani limetoa ruzuku kwa awamu ya pili sasa wilayani Mbarali katika kilimo cha mpunga lengo likiwa ni kuboresha uzalishaji wenye tija ikiwa ni pamoja na kuwapo kwa mashine za kisasa za ukoboaji na maghala ya kuhifadhia baada ya mavuno.

Elias Bange, Diwani wa Kongoro- Mswisi, alisema ruzuku hiyo iwe chachu kwa kampuni husika kuhakikisha walengwa wanafikiwa na kuzalisha kwa kuzingatia teknolojia za kisasa za kilimo cha mpunga ili kuendelea kuwavutia wadau.

Aliiomba kampuni hiyo kuwasaidia wakulima masoko ili kuuza mazao na kupata tija ya mazao wanayozalisha sambamba na matumizi bora ya teknolojia za kisasa za kilimo kwa wakulima.



## Wizara yawataka wazazi kuzingatia mwongozo corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mohammed Nassor Salim, amewataka wazazi na walezi kushirikiana na Wizara kwa kufuata miongozo inayotolewa kuhakikisha watoto wao wanapata elimu bora katika kipindi cha corona.

Mwalimu Mohammed aliyasema hayo katika kikao cha kutathmini matokeo ya utafiti wa elimu kutokana na janga la corona.

Kikao hicho kiliwahusisha walimu wakuu, kamati za maendeleo ya shule na wadau wa elimu katika ofisi za wizara kisiwani Pemba.

Alisema kutokana na Serikali kutangaza wimbi la tatu la corona, ipo haja kwa wazazi na walezi kuiunga mkono wizara kwa kutoa elimu kwa vijana ili kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema Wizara imepanga mikakati maalum kwa ajili ya kuchukua tahadhari ya kuzuia maambukizi yanayotokana na mikusanyiko ya watu, ikiwamo kuboresha uandaaji wa vipindi vya kufundisha watoto, vinavyotolewa katika vyombo vya habari.

"Elimu iliathiriwa na ugonjwa wa corona kutokana na kukosa tahadhari za mapema kwa vile ugonjwa huu ulivamia tu hapa nchini, lakini kwa sasa tumejipanga vizuri kuthibiti athari hizo zisije kujitokeza tena," alisema.

Naye ofisa ufuatiliaji wa takwimu wa wizara hiyo, Salum Mohammed Abdallah, alisema athari kubwa ya elimu iliojitokeza katika takwimu ya mripuko uliopita, inatokana na ufuatiliaji mdogo kwa baadhi ya wazazi kwa watoto wao, jambo ambalo limepelekea watoto hao kuwa na ushiriki mdogo wa masomo.

Aidha, alisema atahakikisha maagizo yaliyotolewa katika kikao hicho atayachukua na kuyafikisha sehemu husika ili kufanyiwa kazi kwa lengo la kuweka tahadhari ya kudhibiti athari zilizojitokeza zisiendelee.

Walimu walioshiriki kikao hicho waliiomba wizara kufanya marekebisho ya uandaaji wa vipindi hivyo.

# Waziri ataka kasi katika ujenzi gereza la watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Mohammed, amewataka wasimamizi wa mradi wa ujenzi wa kituo cha huduma za kurekebisha watoto kumaliza ujenzi huo kwa mujibu wa makubaliano ili lengo la mradi lifikiwe.

Waziri Masoud aliyasema hayo, alipokuwa akizungumza na maofisa na wapiganaji wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar (Magereza), baada ya kukagua ujenzi wa kituo cha huduma za kurekebisha watoto kilichopo Hanyegwa Mchana, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kwa mujibu wa mradi ni kumalizika Septemba mwaka na kusisitiza ukamilishaji huo kuendana na thamani halisi ya fedha zitakazotumika.

Alisema, dhamira ya kujengwa kwa kituo hicho ni kupunguza msongamano kwa sasa hasa watoto ambao wamekuwa wakichanganyika na wafungwa wakubwa.

Aidha, alisema kuwa pia chuo hicho baada ya kumalizika kitatumika kwa wafungwa wakubwa ambao wanatumia vifungo vya muda mfupi na wenye mahitaji maalum.

Waziri huyo alieleza kuwa gereza hilo baada ya kumalizika litakuwa la kisasa na wafungwa watakaopelekwa katika gereza hilo watajifunza stadi za maisha kwa utaratibu mzuri pamoja na maeneo yao watakayotumia yatakua na mazingira mazuri tofauti na magereza mengine.

Hivyo, aliwasisitiza wasimamizi wa ujenzi huo kuzingatia makubaliano hayo ili lengo lifikiwe na kuanza kazi.

Naye, Kamishna wa gereza, Khamis Bakari Khamis, aliahidi kuyafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na waziri na kusema kuwa watayatekeleza kwa muda uliopangwa na endapo kutakuwa na changamoto watazipeleka wizarani.

Mradi huo ulianza mwaka 2016 ambapo ulitarajiwa kumalizika mwaka jana na hadi sasa umekamilika kwa asilimia 98.



Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Jamal Kassim Ali (kushoto), akiuliza swali kwa mkusanyaji mapato wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii alipofanya ziara katika Ofisi za wakala huo, Mazizini Mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bidhaa za mil. 30.7/- zateketezwa Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BIDHAA mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya Sh. 30, 710,000 ikiwamo mchele tani 5.6 zimeteketezwa na Tume ya Ushindani wa Biashara na Kumlinda Mtumiaji Pemba, baada ya kuonekana hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya uteketezaji wa bidhaa hizo huko Pujini Kisiwani Pemba, Mkurugenzi wa Idara ya Kumlinda Mtumiaji wa Bidhaa Bandia na Huduma kutoka tume hiyo, Alie Emanuel Juma, alisema bidhaa hizo zilikusanywa kutoka masoko mbalimbali. Alisema idara hiyo imekuwa ikifanya msako katika masoko na kwa wafanyabiashara ili kuangalia ubora wa bidhaa na kulinda afya ya mtumiaji, ambapo bidhaa zilizoteketezwa zilikusanywa katika ukaguzi kwa kipindi cha Aprili na Juni 2021.

Alieleza kuwa uteketezaji wa bidhaa kama hizo hauna muda maalumu, isipokuwa unafanyika baada ya kugunduwa bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Alieleza kuwa mchele ulioteketezwa haukuwa umeisha muda wake wa matumizi, lakini ulikuwa umeshaharibika ambao haufai kwa matumizi ya binaadamu na Serikali imeagiza uondolewe sokoni.

Alieleza kwa vile wao wana sheria inayowataka kufanya kazi hizo ikiwamo Sheria namba 5 ya mwaka 2018, imewapa mamlaka ya kuondoa sokoni bidhaa yoyote ambayo imepitwa na muda na zisizo salama na haifai kwa matumizi ya binadamu chini ya kifungu cha 63 na 64.

Aliwataka wafanyabiashara kuwa waangalifu wa kutunza bidhaa katika maghala kwani wengi uhifadhi wao sio mzuri.

Aliwashauri wananchi wanapokwenda dukani kununuwa bidhaa kabla ya kutoa fedha wawe na utamaduni wa kuangalia tarehe ya matumizi.

Naye Ofisa kutoka Tume hiyo Pemba, Ali Omar Massoud, alisema ni vyema wananchi wakawa waangalifu kutumia bidhaa zilizokuwa zimeshapitwa na wakati ili kuepuka madhara.

Kwa upande wake, Naibu Sheha wa Shehia ya Pujini,Shaib Haji Faki, aliwataka wananchi kuwa makini kununua bidhaa ambazo zimeshapitwa na muda wa matumizi, kwa sababu zitawasababishia maradhi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA ZINAUZWA

NYUMBA ZIPO 3 KATIKA ENEO MOJA MAHALI KIBAHA MAILI MOJA UKUBWA 25M X 25M INAVYUMBA 11,VYUMBA 7 VINAJITEGEMEA NA CHUMBA NA SEBULE VIWILI,INATYLES,MADIRISHA ALUMINIUM NA BATI LA MSOUTH,MAJI NA UMEME VIPO,DOCUMENT MAUZIANO YA SERIKALI ZA MITAA

**MAWASILIANO:0768 909866**

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 18/08/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA KIWANJA KILICHOPO MTUMBA BLOCK 'EE' PLOT NO.648, UKUBWA (SQM 648) MALI YA JANE BUSHIRI, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA KIWANJA KILIPO, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

116369602

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841**

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 18/08/2021 SAA MBILI ASUBUHI WA KUUZA KIWANJA KILICHOPO MTUMBA BLOCK 'AL' PLOT NO.244, UKUBWA (SQM 1303) MALI YA ERICK AYILLA, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA KIWANJA KILIPO, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

116369602

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841**

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 18/08/2021 SAA TANO ASUBUHI WA KUUZA VIWANJA VILIVYOPO MTUMBA BLOCK 'TT' PLOT NO.1008, UKUBWA (SQM 928) MALI YA PROCHES MARANDU NA PAULO KATYEGA BLOCK NO 'MM' PLOT NO 42, UKUBWA (SQM 921), BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MIKOPO WALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA VIWANJA VILIPO, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE

116369602

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841**

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 18/08/2021 SAA TISA MCHANA WA KUUZA KIWANJA KILICHOPO BUIGIRI BLOCK 'A' PLOT NO.1016, UKUBWA (SQM 523) MALI YA MARK ITALLANGE, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LTD, S.L.P.4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA KIWANJA KILIPO, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

116369602

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841**

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD &COURT BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 17/08/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA TOYOTA PORTE T 436 DFB, MALI YA PETER KASWAMILA MGETA, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA GK FINANCIAL SERVICES LIMITED, P.O.BOX 1685 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

116369602

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0713913150/ 0688729841**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

DORISS SWAI MALLYA ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 517 CCW TOYOTA VITZ. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: DAR/URA/RB /359839/2021.

116368602

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.223/2021**

Ombi la **ESTER JAMES NG`OWO** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **CYRIL JONATHAN MPOTO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 04/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 20/07/2021**

116369402

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.204/2021**

Ombi la **MASHAKA SAID CHANDE** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **SALIMA MASHAKA CHANDE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 02/08/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 08/07/2021**

116369902

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.225/2021**

Ombi la **NEEMA JACKSON NELINGWA** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **JULIAS VITALIS SHIRIMA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 12/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 20/07/2021**

116368702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi No. 104/2021**

**Ombi la FELICIAN VERIDIAN LWIZA Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu ADVERA ISACK NTINABO**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 12/8/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 22/7/2021.

116370602

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**
**LAND CASE APPEAL NO. 114/2020**
**(Arising from MULEBA DLHT APPLICATION NO. 20/2020)**

**JOSEPH JACOB BYASHAO.........................................APPLICANT**

**VERSUS**

**MESHACK OBADIA KANYAMBO & 2 OTHERS...........RESPONDENT**

**TO, 1. PAULETHA GIDION**
**2. BUHAYA VILLAGE COUNCIL**

**RE: NOTICE FOR DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned appellant has lodged a case registered as Land case appeal No. 114/2020 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 10th day of August, 2021 at 9:00 am before Hon. A. MWIPOPO J. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this **14th day of July, 2021.**

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

116369502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 89/2021**
**MDAI KULWA JOHN MSAMBILI**
**DHIDI YA**
**MDAIWA MWAJENI HAMIS**

**KWA MWAJENI HAMIS, AREA 'C'**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA Tsh. 850,000.**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe 02/08/2021 saa mbili asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shauri hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 20/07/2021.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

116369302

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARIAM .A. LUGONO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5164/0023** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ST. MARCUS SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/361125/2021.**

116370002

---

## TANGAZO KUPOTEA KADI YA BAJAJI

**Martin Charles Fungameza** mkazi wa Ndala Manispaa ya Shinyanga. Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 216 BRR** aina ya **TVS** yenye jina la Hellen Kiseru Amour ambayo ilipotea wilayani Mpanda.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Martin Charles Fungameza kwa simu namba **0752070218.**

**RBnamba/ KAT/MPA/RB/234241/2021.**

116370702

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NDEAKEMFOO NDEMFOO SHOO**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **TOYOTA COASTER**, Yenye namba za usajili **T 828BRN .** Yenye Chassis namba **HDB300001041** na Injini namba **1HD1041** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi Taarifa : **KIL/HAI/RB/354038/2021**

116370102

---

## KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TANGAZO

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## OPPORTUNITIES FOR INTERNSHIP AT ATCL

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is a legal entity owned by the Government of the United Republic of Tanzania and established under section 4 (1) of the Air Tanzania Corporation (Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities) Act, Cap. 205 R.E of 2002 and incorporated under the terms of The Companies Act, Cap 212, Act No. 12 of 2002.

**Intern Details:**
Applications are invited from suitably qualified Tanzanian graduates for internship in the following areas/programs at ATCL;

1. **Aircraft Maintenance (4 Positions)**
   **Minimum Requirement:**
   - Bachelor Degree of Aeronautical Engineering or equivalent qualification from a recognized institution.
2. **Customer Service and Reservation (4 Positions)**
   **Minimum Requirement:**
   - IATA Diploma in Reservation and Ticketing
   - Bachelor Degree of Business Administration and Marketing from a recognized institution is preferable.
3. **Cargo Sales (5 Position)**
   **Minimum Requirement:**
   - Trained /qualified in Cargo operations (IATA Diploma in Cargo, Dangerous goods Regulations) or Diploma or Degree in Air Transport management.
4. **Traffic Liaison (4 Positions)**
   **Minimum Requirement:**
   - Diploma in Air Transport Management or IATA Diploma in Ground Handling Services or equivalent qualification from a recognized institution.
5. **Aviation Quality and Safety (4 Positions)**
   **Minimum Requirement:**
   - Certificate in Flight Operation or Airline Quality and Safety from a recognized institution.

**Other Requirements:**
- Possession of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) is a must.
- Computer literacy (E.g. Ms. Word and Excel).
- Good communication (English and Swahili) and Interpersonal Skills.
- Excellent analytical skills.
- Must be ready to adhere to ATCL internal guidelines.

**Mode of Application**
Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the applications attached with the following:

i. A detailed curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including Secondary School), other relevant certificates and licenses. **(Tanzanian applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities. i.e. Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Examination Council (NECTA).**
iii. Two recent passport size photographs,
iv. Names and addresses of at least two reachable referees,
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone numbers.

**Note: - Misrepresentation of facts and qualifications during application shall warrant legal consequences.**

**Closing Date**
Application letters should reach the undersigned **within 14 working days from the first date of this announcement: -**

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543,**
**DAR ES SALAAM**
**DATE ISSUED: 23.07.2021**

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## VACANCIES ANNOUNCEMENT - READVERTISED

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is making some reforms in its structure, internal operations and staffing to accommodate business needs. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following position.

**1. EXECUTIVE ASSISTANT (1 POST)**

**(a) Qualifications**
- At least a Form IV Certificate with a Diploma in Secretarial Studies.
- Must have passed Shorthand and Hatimkato 80 -100 w.p.m
- Must have attended Management Development Course for Executive Assistants Level I or relevant qualifications
- Hands on Working experience of not less than five (5) years in a reputable organization
- Outstanding command in communication both in English and Kiswahili (writing and speaking)
- Candidates with a strong background in working in competitive business environment with heavy administrative workload as well as handling Senior Executives will be given preference

**(b) Duties and Responsibilities**
- Providing assistance to top executives of the Company
- Assisting in coordinating secretarial functions with other departments.
- Typing letters and other documents
- Undertaking routine correspondence with prior approval of his/her senior.
- Arranging meetings and appointment schedules for the Senior Executives.
- Assisting in drafting and proof – reading reports and write-ups for the executives.
- Coordinate official appointments and travel arrangements
- Deals with confidential matters in the office of the Executives.
- Keep record of events and documents
- Performs any other duties as may be assigned by his/her senior.

**2. REMUNERATION:**
Five 5) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Scales and Incentive Scheme.

**3. MODE OF APPLICATION**
Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i) A curriculum vitae (CV),
ii) Certified copies of all certificates (including secondary school), other relevant certificates/licenses. Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii) Two recent passport size photographs
iv) Name and address of at least two reputable referees;
v) Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other fact/information on application shall warrant legal consequences.**

**4. CLOSING DATE:**

The application letters should reach the undersigned within **14 days** from the first date of issue of this announcement.

The application letters should be directed to the following address: -

**MANAGING DIRECTOR & CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543, DAR ES SALAAM**
**23.07.2021**

BancABC part of atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Mar-21 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,762 | 3,013 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,864 | 11,430 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 42,827 | 44,150 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 5,883 | 3,830 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 105,943 | 104,467 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 125,435 | 130,214 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 25,783 | 26,974 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6,827 | 6,231 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **328,325** | **331,310** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 101,584 | 104,164 |
| 18 | Amana za Wateja | 110,991 | 111,016 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,464 | 1,842 |
| 28 | Madeni | 76,856 | 75,705 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **290,894** | **292,727** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **37,431** | **38,584** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Hifadhi isiyosambazwa | 1,716 | 1,716 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (86,263) | (86,263) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,965) | - 812 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 989 | 989 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **37,431** | **38,584** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 2,374 | 2,618 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 19,109 | 21,126 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 12,796 | 15,127 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.40% | 11.65% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.82% | 14.54% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 65.03% | 67.54% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 38.20% | 39.30% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 49.18% | 47.89% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.21% | -1.16% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.90% | -1.03% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 9,931 | 10,642 | 20,065 | 20,887 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,954) | (4,678) | (9,786) | (9,429) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **4,977** | **5,964** | **10,278** | **11,458** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 259 | - | 859 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 36 | (106) | 113 | (524) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,040** | **844** | **2,291** | **1,916** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 215 | 223 | 507 | 703 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 234 | 169 | 434 | 350 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 591 | 451 | 1,351 | 864 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,186)** | **(7,277)** | **(14,536)** | **(14,625)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,524) | (2,486) | (5,098) | (5,021) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,663) | (4,792) | (9,437) | (9,604) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,134)** | **(316)** | **(1,853)** | **(915)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (19) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,153)** | **(350)** | **(1,965)** | **(983)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,153)** | **(350)** | **(1,965)** | **(983)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 161 | 167 | 161 | 167 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | -47% | -14% | -20% | -10% |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.70% | -0.22% | -1.19% | -0.62% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -6.07% | -1.63% | -10.34% | -4.59% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 119.44% | 106.89% | 115.64% | 109.35% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.41% | 1.82% | 2.92% | 3.49% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-21 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-21 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,134) | (719) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 803 | 886 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 4,778 | 3,738 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (2,605) | (2,527) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 1,324 | (972) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (378) | (1,171) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,191 | 829 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (19) | (93) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **3,960** | **(30)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,399) | (534) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,399)** | **(534)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 1,150 | 1,065 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **1,150** | **1,065** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 3,711 | 501 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 122,741 | 122,240 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **126,452** | **122,741** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2021

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (86,262) | 1,716 | - | 989 | 39,396 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (1,965) | - | - | - | (1,965) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (88,228) | 1,716 | - | 989 | 37,431 |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (80,525) | 130.00 | - | 1,065 | 43,623 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (4,152) | - | - | - | (4,152) |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (1,586) | 1,586 | - | (76) | (76) |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (86,262) | 1,716 | - | 989 | 39,396 |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 22nd July 2021 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 22nd July 2021 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 22nd July 2021 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 22nd July 2021 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 22nd July 2021 |

216370501

BancABC part of atlasmara

# MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| | | | |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| | | | |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| | | | |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |

| **CORPORATE BANKING** | | | |
|---|---|---|---|
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| | | | |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| | | | |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| | | | |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| | | | |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| | | | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| | | | |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

216370501

## KWA UFUPI

### CHELSEA YAJITOSA

CHELSEA imezungumza na wakala wa mshambuliaji wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 32, kuhusu uwezekano wa kumleta Stamford Bridge. (**Bild, via Sun**)

### RAMSDALE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kuwasilisha dau la pauni milioni 30 kumnunua kipa wa Sheffield United, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 23. (**TalkSport**)

### ABRAHAM AGEUKA LULU

CHELSEA iko tayari kumwachia mshambuliaji, Tammy Abraham kujiunga na mahasimu wao wa Ligi Kuu England, Arsenal kwa mkopo. Tottenham na West Ham pia wanamnyatia nyota huyo mwenye umri wa miaka 23. (**Sun**)

### WERNER NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, ameanzisha mazungumzo ya kuondoka Chelsea msimu huu wa joto. Kuna uwezekano akarejea katika ligi yake nyumbani, Bundesliga. (**90min**)

### LIVERPOOL KUUZA NYOTA

LIVERPOOL huenda ikawauza nyota wao, Nat Phillips mwenye umri wa miaka 24, winga wa Wales, Harry Wilson mwenye miaka 24, mshambuliaji wa Ubelgiji, Divock Origi (26), Neco Williams miaka 20 na kiungo, Xherdan Shaqiri (29), katika mpango wa kukusanya kati ya paundi milioni 60 hadi 70. (**Liverpool Echo**)

### PSG YAKOMAA NA POGBA

KLABU ya Paris St-Germain inamtaka kiungo wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, lakini klabu hiyo itahitajika kuwauza baadhi ya wachezaji wake kwanza. (**Sky Sports**)

### UNITED YAMTAKA NEVES

MANCHESTER United wako mbele ya Arsenal katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 24, kwa kiasi cha pauni milioni 35 kutoka Wolves msimu huu wa joto. (**TalkSport**)

### GORETZKA ANUKIA MADRID

KLABU ya Real Madrid inawaniwa kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Leon Goretzka mwenye umri wa miaka 26.(**Daily Mail**)

### CANTWELL SOKONI

ASTON Villa wamepiga hatua katika mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Norwich City, Todd Cantwell mwenye umri wa miaka 23. (**Football Insider**)

### PALACE YAMTAKA KABAK

KLABU ya Crystal Palace inajadiliana na Schalke kuhusu mkataba wa mlinzi wa Uturuki, Ozan Kabak mwenye umri wa miaka 21. Huenda akagharimu kati ya pauni milioni 10 hadi 12. (**Guardian**)

### LINGARD AWINDWA

EVERTON imeungana na orodha ya klabu mbalimbali za Ulaya zinazofuatilia hatima ya mshambuliaji, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28 na klabu yake ya Manchester United. (**Sun**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD ANATAKA KUREJEA CHELSEA

**●●● Ajitabiria kiwango chake kurejea na kusahau majeruhi ya mara kwa mara ambayo...**

**MADRID,** Hispania

EDEN Hazard ametajwa anavutiwa na uamuzi wa kurejea Chelsea msimu huu wa joto, ikiwa ni miaka miwili tangu alipoondoka Stamford Bridge na kuungana na Real Madrid.

Hazard alitumia miaka saba kuichezea Chelsea, kabla ya uamuzi wake wa kuondoka, tangu alipojiunga mwaka 2012 akitokea Lille ya Ufaransa.

Akiwa na The Blues hao alicheza jumla ya mechi 352 na kufunga mabao 110 katika mashindano yote, akifanikiwa kutwaa mataji mawili ya Ligi Kuu England, Kombe la FA, EFL na mataji mawili ya Ligi ya Europa.

Real Madrid walitumia takribani pauni milioni 103.5 kwa nyota huyo wa Ubelgiji mwaka 2019, lakini amecheza mechi 30 pekee kwa misimu yote akiwa nchini Hispania.

Taarifa iliyoripotiwa na The Mirror, imesema nyota huyo mwenye miaka 30 sasa anataka kurudi tena London na kurejea kwenye kiwango chake kama awali.

Hata hivyo, haijawa wazi kama Thomas Tuchel anaweza kuwa na nia ya kumrejesha pale Stamford Bridge.

Hazard amevumilia wakati mgumu wa kuuguza na majeraha mara kwa mara tangu alipowasili mji mkuu wa Hispania, Madrid akitokea England.

Hata hivyo, gazeti la Marca liliripoti kwamba Real Madrid imejiandaa kumweka Hazard sokoni kwenye dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto licha ya nia ya kocha mpya, Carlo Ancelotti kutaka kufanya kazi na raia huyo wa Ubelgiji.

Ripoti hiyo inadai Ancelotti hana uhakika kama anaweza kumtumia vyema mshambuliaji huyo aliyetawaliwa na majeraha misimu miwili mfululizo iliyopita, lakini Real Madrid wanaweza kuwa tayari kumuuza ikiwa watapata mnunuzi kwa bei sahihi.

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO FC KUWABEBA NYOTA WAZAWA 2021/22

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Namungo FC umesema ili kuwa na kikosi imara kuelekea katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22, wanahitaji kusajili wachezaji wapya saba ambao watakiongezea nguvu kikosi chao.

Mapendekezo ya kusajili nyota hao yameandikwa katika ripoti ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Suleiman, alisema tayari viongozi wameshaiangalia ripoti hiyo na wanaahidi kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyowasilishwa ili kufikia malengo.

Suleiman alisema kwa kufuata mahitaji ya kocha, wanaamini watakuwa na kikosi imara kitakachoonyesha ushindani katika kila mechi watakayocheza.

Kiongozi huyo alitaja nafasi ambazo wanahitaji kusajili kwa mujibu wa ripoti ya benchi lao la ufundi ni pamoja na washambuliaji wawili, kiungo namba nane na sita, beki wa kati pamoja na beki wa kushoto.

"Tayari viongozi wameanza kufanyia kazi ripoti ya mwalimu ambayo hasa inajikitika katika suala la usajili, tutaangalia zaidi wachezaji wa ndani ambao Kocha Mkuu (Morocco), amewataka na atawataja kwa majina na nafasi zao, wote tumeanza kufanyia kazi," alisema katibu huyo.

Alisema pia leo wanatarajia kutangaza majina ya wachezaji ambao wataachana nao ikiwamo waliomaliza mikataba ili kuwapa nafasi ya kwenda kujiunga na klabu nyingine.

"Tutawapa taarifa rasmi kama taratibu zinavyoelekeza, tunajua lazima maisha yaendelee na kwa kufuata kanuni tutalitekeleza hilo bila kuathiri upande wowote," Suleiman alisema.

Aliongeza kwa sasa wachezaji wao wamekwenda mapumziko lakini watarejea baada ya muda mfupi ili kuanza kujipanga kuelekea msimu mpya.

"Tayari wachezaji wamepewa likizo kuanzia Jumatatu iliyopita, watapumzika siku 10 na baada ya hapo timu itaingia kambini ili kuanza maandalizi mapya," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza wanatarajia kuanza kuweka kambi katika maskani yao Ruangwa, Lindi na hapo baadaye watahamia mahali kwingine ambapo uongozi utaridhia.

Namungo imemaliza msimu uliopita ikiwa katika nafasi ya tano lakini ikitinga hatua ya makundi kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot, Abdallah Saad, akiwa ameshikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 6.6 baada ya kubashiri kwa usahihi matokeo ya mechi 11 kati ya 13 za Jackpot ya SportPesa. Zawadi ya Jackpot wiki hii ni Sh. milioni 382.1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanuni za soka Z'bar kuboreshwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WADAU wa soka wa visiwani hapa wametakiwa kuwasilisha maoni mbalimbali kwa ajili ya kuboresha kanuni za msimu ujao wa Ligi Kuu Zanzibar 2021/22, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Haji Issa Kidali alisema mwisho wa kupokea maoni ya wadau hao ni leo jioni.

Kidali alisema anahitaji kuona wadau wanashiriki kikamilifu katika mchakato huo ili kuwa na kanuni imara za ligi hiyo ya juu Zanzibar.

"Bado mwamko ni mdogo kwa wadau wa soka katika kutoa maoni yao hali ambayo baadaye inaweza kuleta malalamiko, na wadau hao hao wanakuwa mstari wa mbele kukosoa kanuni ambazo zinatolewa," alisema Kidali.

Kiongozi huyo alisema ZFF imeamua kupitia kamati ya mashindano imeamua kutoa fursa kwa wadau kutoa maoni ili kuziboresha kanuni ziendane na soka la sasa.

"Tunataka kuwa na kanuni shirikishi ili kuondoa migogoro ambayo mara nyingi hujitokeza kutokana na upungufu wa kanuni zetu ikiwamo suala la rufaa, lakini pia tutaendelea kupokea maoni kutoka katika vyama wanachama wa ZFF," Kidali alisema.

## Boomplay yazidi kujikita Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Boomplay, App inayoongoza barani Afrika kwa utoaji huduma ya kusikiliza na kupakua muziki na Clouds Media Group (CMG) zimesainia mkataba wa ushirikiano wa kimkakati ambao utawawezesha watumiaji wa App hiyo kupata maudhui kutoka Clouds FM.

Kupitia ushirikiano huu, watumiaji wa Boomplay duniani kote watakuwa na uwezo wa kusikiliza vipindi pendwa kutoka Clouds FM ikiwamo XXL, Amplifaya, Traffic Jamz, Bongo Fleva na vingine vingi.

Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli amesema hayo jana baada ya kampuni hizo kufikia makubaliano rasmi.

"Mara zote tumekusudia kuendelea kuwaunganisha wasikilizaji kupitia App yetu na matumaini yetu ni kuwafikia wasikilizaji wengi zaidi kupitia vipindi pendwa vya Clouds FM. Pamoja na wasikilizaji wengi wa redio hiyo kuwa vijana, ushirikiano huu utatengeneza uwanja mpana wa kuwaunganisha vijana hao kupitia ulimwengu wa Boomplay, mahali ambapo wasikilizaji wanahudumiwa kwa ubora zaidi kupitia huduma za muziki na uzoefu wa kutosha," alisema Stambuli.

Aliongeza Boomplay itaendeleaza ushirikiano wenye tija ili kuweka vizuri mazingira yake ya kidijitali na vilevile kuunganisha mitiririko bora wa maudhui pendwa wakati wowote na popote duniani.

Naye Ofisa Mkuu wa Ubunifu na Mkakati wa Clouds Media Group, Reuben Ndege aliipongeza kampuni hiyo kwa kuongoza katika utoaji wa maudhui mbalimbali barani Afrika.

"Ushirikiano huu una maana kubwa kwetu, kwani unaturuhusu kuwa karibu na wasikilizaji wetu ambao wengi wao ni vijana na kupitia mamilioni ya watumiaji wa Boomplay tutaweza kuwafikia vijana wengi zaidi nchini Tanzania na duniani kote," Alisema Ndege.

Ofisa huyo alisema pia ushirikiano huo utasaidia kubadilisha maudhui yetu kwa wasikilizaji kutoka katika kupanga kusikiliza kwenda kwenye usikilizaji wa muda wowote ambapo msikilizaji hatokosa sauti tulivu, inayopendwa, ya kipekee, inayobadilika na kusambazika ambao ndio utamaduni wa maudhui ya Clouds Media.


Aliongeza hakuna mshirika mwingine waliyemfikiria katika ushirikiano huo wa kimkakati zaidi ya Boomplay.

Aliongeza ushirikiano huo ni wa kwanza wa aina yake na Clouds Media inakuwa kampuni ya kwanza ya vyombo vya habari kushirikiana na Boomplay kwa Afrika Mashariki.

# Michezo

Ijumaa Julai 23, 2021

Nipashe


## HAZARD ANATAKA KUREJEA CHELSEA

HABARI UK. 22



Mashabiki wa Yanga waliojitokeza kuipokea timu yao (ndani ya basi kushoto), baada ya kuwasili Kigoma jana asubuhi kwa ajili ya mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba itakayochezwa keshokutwa Jumapili kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani humo. **PICHA: MTANDAO**

## Okwi safari imeiva

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA mshambuliaji wa Simba, Emmanuel Okwi anatarajiwa kutua nchini wiki ijayo kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo ya kurejea kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Okwi atatua nchini akitokea kwao Uganda ambapo alirejea tangu mwezi uliopita baada ya kumaliza mkataba na klabu yake ya El Itihad ya Tunisia.

"Nimezungumza na Okwi na amenieleza anakuja nchini mapema wiki ijayo, naamini anarudi nyumbani," kilisema kwa kifupi chanzo chetu.

Hata hivyo Okwi alishindwa kusema anakuja nchini kukamilisha mazungumzo au ameshamalizana na waajiri wake hao wa zamani.

"Ninasubiria tu muda," Okwi alisema kwa kifupi jana.

Tayari TFF imeshafungua dirisha la usajili kwa wachezaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo litafungwa rasmi ifikapo Agosti 31, mwaka huu.

# SIMBA, YANGA ZAAMSHA SHANGWE

### Mashabiki wao wapishana Uwanja wa Ndege Kigoma, majigambo yatawala...

**Na Saada Akida**

MAMIA ya mashabiki wa Simba na Yanga kutoka sehemu mbalimbali za mji wa Kigoma walijitokeza kwenye Uwanja wa Ndege kwa ajili ya kuwapokea wachezaji na viongozi wa timu hizo ambao waliwasili mkoani humo tayari kwa mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika.

Yanga ndio ilikuwa ya kwanza kufika Kigoma ambapo ilitua saa 02:10 asubuhi wakati watani zao waliwasili mkoani humo jioni.

Hata hivyo Yanga ilitua Kigoma bila ya mshambuliaji wake, Michael Sarpong na beki, Abdallah Shaibu 'Ninja' ambao ni majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya kutua Kigoma, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi alisema anatarajia mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa hali ambayo inamlazimu kubadili mfumo kwa wachezaji.

Nabi alisema mbali na kujipanga kuingia uwanjani tofauti na walipokutana na Simba katika mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara, analazimika kubadlisha mfumo wa uchezaji kwa sababu ya 'ugumu' wa uwanja.

Kocha huyo alisema lengo la kubadili mfumo ni kuifanya fanali hiyo iwe rahisi kwao na hatimaye lengo la kupata matokeo chanya likamilike na hatimaye kumaliza msimu kwa furaha.

"Hautakuwa mchezo rahisi, Simba ina wachezaji wazuri na wamejipanga kulingana na matokeo ya mechi iliyopita, wao watahitaji kupata matokeo kama ilivyo kwetu, tumejiandaa kupambana ili kushinda na kuondoka na Kombe la FA, tunatakiwa kuwa makini na kuhakikisha tunaweka sawa mambo ya kiufundi vyema, tunahitaji ushindi tu," alisema Nabi.Aliongeza kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea fainali hiyo ili malengo yao ya kutwaa taji hilo baada ya kushindwa kuivua Simba ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wanaushikilia kwa msimu wa nne mfululizo yatimie.

Nabi alisema anawaheshimu Simba na anafahamu wapinzani wao ambao walikuwa na matokeo mazuri katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliomalizika.

> **"Tutaingia uwanjani kiving ine, tunajua umuhimu wa kombe hili, tumejipanga vi zuri kukabiliana nao, hatut abweteka," Nabi alisema.**

Ofisa Mtendaji wa Simba, Barbara Gonzalez aliliambia gazeti hili kikosi chao kimetua salama Kigoma na wamekwenda kwa kazi moja ya kuhakikisha wanamaliza msimu kwa shangwe.

Barbara alisema wachezaji wote wana ari na kiu ya kusaka matokeo chanya dhidi ya watani zao Simba na hatimaye kuwafuta machozi mashabiki wao ambao waliumia baada ya kufungwa kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kufungwa bao 1-0.

"Bado hatujasahau maumivu, tumekuja Kigoma kusaka ubingwa na kukamilisha hesabu, tunalihitaji zaidi kombe hili, hatuko tayari kupoteza mchezo huu wa Jumapili," Barbara alisema.

Wakati huo huo, uongozi wa Yanga umetoa malalamiko kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kutokuwa na imani na mwamuzi, Ahmed Arajiga kutoka Manyara ambaye ameteuliwa kuchezeshaa 'dabi' hiyo ya keshokutwa.

Yanga katika taarifa yake imesema Arajiga amehusika katika mechi za Simba kuanzia hatua ya robo fainali, nusu fainali hivyo wanashangaa kuona amepangwa tena kusimama katikati kwenye mchezo huo wa fainali.

"Tunaomba TFF na menejimenti ya mashindano haya kutafakari juu ya uamuzi wa kumtumia mwamuzi huyu katika mchezo huo mkubwa wa fainali," ilimaliza taarifa hiyo ya Yanga.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >